# Sababu Sita Za Kusudi La Gabrieli Kumzuru Danieli

Jeffersonville, Indiana, USA

Julai 30, 1961J

1 Lakini nilishangazwa sana kwa ninii…watoto wetu matineja asubuhi ya leo, watoto wadogo, mwajua, kadogo "fefe" na "fifi," kadogo, wale ninii…wajua, wa kumi na sita. Nao wanakuja kanisani, mwajua, kuhusu … Wasichana wadogo, kwenye umri huo, wanataka waonekane wanapendeza, mnajua. Nao, mnajua, nywele zote zimesokotwa viwimbiwimbi, juu ya vichwa vyao; niliwaona, nami nilipokuwa nikihubiri, ziliendelea tu kusinyaa, na kusinyaa. Na, muda si muda, walikuwa wanazitimua zirudi nyuma zitoke usoni mwao, viwimbiwimbi vyao vyote vikanyoshwa.

2 Msichana mdogo wa Dada Downing, na—nami nikamwona. Na mdogo—mdogo—mdogo … Mtoto wa Ndugu Collins… Jina lake ni nani? Mdogo … [Mtu fulani anasema, "Betty." — Mh.] Betty, Betty mdogo. Kwa namna fulani nilicheka kidogo, peke yangu. Lakini niliona uzuri wote huo, wajua, zimefungwa vizuri kabisa, na halafu mara moja zikaninii…

Vema, nawatakieni heri, vipenzi, mnapendeza, kwangu mimi, hata hivyo. Hiyo ni kweli. *Uzuri*, ni—ni roho nzuri itakayokuja na kuketi katika mkutano namna hiyo, na kusikiliza Injili. Hilo ndilo linalomfanya msichana kuwa mzuri. Nami nafikiri mvulana yeyote halisi, anayestahili kuoa, anafikiria jambo lile lile. [Ndugu Neville anasema, "Amina." — Mh.] Asante, bwana. Hilo ni zuri. Mtu fulani anakubaliana nami. Hiyo, hiyo ni kweli. Vema. Ninaamini ya kwamba hiyo ni Kweli.

3 Sasa hilo si ni la ajabu? Nilifungua moja kwa moja kwenye Danieli 9 nilipofungua Biblia yangu. Sasa, kwa kawaida ninamwambia kila mtu, wasitoe makoti yao, walio na tobo kwenye shati, kwa hiyo ninatumaini langu halina. Lakini—lakini nimeona wakati ambapo sikuweza kutoa koti langu, shati langu likiwa na tobo, kweli kabisa. Nami nafikiri hili halina.

Sasa, loo, kwangu mimi, sisi…na ninaamini kwa niaba ya wasikilizaji, tunauthamini Uwepo wa Roho Mtakatifu asubuhi ya leo.

Nasi tunafurahia ushirika na uwepo wa mmoja kwa mwingine. "Jinsi lilivyo tamu, jinsi lilivyo zuri, jinsi lilivyo la kupendeza, kwa ndugu kukaa pamoja katika umoja. Ni kama upako mzuri wa mafuta yashukayo ndevuni mwa Haruni, yashukayo mpaka upindo wa mavazi yake."

4 Nilienda kula huko leo, huko Blue Boar, na ni nani niliyemkuta kule ila Ndugu Bill hapa, na Dada Dauch wameketi pale, wa—wakila tu nyama ya kuku wa kukaanga nzuri sana niliyopata kuona, na wakifurahia sana, wakikazana kuila kabisa, wajua. Nilienda kwenye orofa ya juu na nikakutana na sehemu kubwa ya kanisa kule juu, nao walitaka hata kunilipia chakula changu cha jioni. Sasa, hilo lilikuwa ni jambo zuri sana, ninathamini hilo.

Nilipofika nyumbani, huyu hapa Billy anakuja na sanduku la nyanya ambazo mtu fulani aliniletea, kutoka huko mbali katika lile jimbo zuri, baridi baridi la Georgia kule chini, ambako kuna hali ya baridi kidogo kule, wananiambia, kwenye wakati huu.

5 Ndipo, nikakutana na jamaa mdogo huko nje. Nilikuwa nikitoka kwenye mazungumzo yangu ya faragha, alasiri ya leo, na nikishuka kuja kupitia kanisani kama nusu saa iliyopita, na maskini…ni jamaa mdogo hivi, nje, akasema… Nikasema, "Kuna joto."

Akasema, "Ni choto kweli!" Nilijua alitoka Georgia, kwa hiyo akasema, "Hakika kuna joto huko Georgia!"

Vema, tunajaribu kutoroka mahali penye joto zaidi, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hilo ndilo lililotuleta hapa.

6 Asanteni sana, marafiki, kwa wema wenu wote. Ningefanya nini bila ninyi? Ni—ningefanya nini bila ninyi? Kama nisingekuwa na mtu aliyenipenda, hakuna mtu ambaye angesikiliza Ujumbe huu, Ujumbe wangu wote haungefaa kitu hata kidogo. Siwezi kulihubiri kwa nguzo za simu na miti. Zisingeuelewa. Kwa hiyo haina budi kuwa ni watu kama ninyi nyote, ambao watakuja na kusikiliza. Na wakati mnapokuja na kuketi mahali penye joto kama hapa, na ni ninii… Mke wangu alisema karibu aungue nyuma kule, asubuhi ya leo. Na kuwaona watu, na wakati mwingine watu wagonjwa, ambao wanaketi kwenye mikutano kama hiyo namna hiyo, Mungu na awape ma—makazi mazuri yanayopendeza sana Utukufuni, ndilo ombi langu. Nami ninatumaini tu na kuamini ya kwamba Yeye atafanya jambo hilo.

7 Sasa, hebu tuone. Koti langu, mtu fulani aliliweka hapa. Nami sina budi kusoma kidogo usiku wa leo. Ni wangapi wanafurahia sehemu za kwanza za huu? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Loo, kama hakungekuwa na joto sana, tungeendelea tu moja kwa moja, moja kwa moja juma lote, pamoja na—na Kitabu cha Ufunuo. Ninakipenda tu. Ninaishi tu ndani Yake. Nanyi ombeni, kwa namna fulani, kwa ajili yangu, juma hili, kwa maana Jumapili ijayo mimi… Bwana akipenda, sina budi kukabiliana na kule, kuweka majuma yale pamoja. Na hilo ni jambo ambalo sijui lo lote juu yake. Na kwa hiyo nitamtumainia tu Bwana ya kwamba itabidi Yeye anipe jibu.

Na ni—nimesoma watu wengi mbalimbali ambao—ambao walinena habari zake, ambao wameandika habari zake. Nimesoma mihtasari iliyoko pambizoni hapa chini, za Dk. Scofield, mwanazuoni mashuhuri, lakini kwa kweli sikuweza kukubaliana naye, katika mihtasari yake mingi ya pambizoni, maana siwezi kuona jambo hilo. Ambapo … Halina budi—halina budi kuifanya ile picha ikae sawa.

8 Sasa, kama ulikuwa unaunganisha mchezo wa zuzua, na muda si muda unajua, useme, "Loo, hiki kinaingia *hapa*. La, nina hakika hiki kinaingia *hapa*." Vema, yakubidi uangalie hapa kwenye picha yako, uone unachofanya. Halafu kama— kama hufanyi jambo hilo, utavuruga mchezo wako kabisa.

Sasa vipi kama ulikuwa uchukue ninii…ungalikuwa na picha adhimu nzuri sana ya mashambani, na ng'ombe akila nyasi kwenye kilele cha mti? Sasa, hilo halingekuwa sawa (sivyo?), maana hali nyasi juu ya mti. Kwa hiyo, hivyo ndivyo ilivyo kama, wewe Roho Mtakatifu hayaunganishi hayo Maandiko pamoja. Ndipo, una picha yote, picha iliyo kuu ya ukombozi. Hivyo ndivyo tunavyotaka, ile Kweli. Na mpaka tutakapojua ile Kweli, tutaliacha tu peke yake. Halafu basi, Mungu atakapotupa ile Kweli, vema, ndipo nitanena habari zake.

9 Unajua nini? Ninadhani Ndugu Roy Slaughter na—na baadhi ya wale watu wa zamani hapa, walioanza huko nyuma muda mrefu uliopita… Kulikuwa na kama, nadhani, miaka ya kwanza mitatu ama minne ya huduma yangu, papa hapa maskanini, hata nisingeweza kuhubiri juu ya somo la kuzimu, kwa sababu si—sikuweza kujua kama palikuwa ni mahali panapowaka moto, kama palikuwa ni kaburi. Na kila wakati Neno liliposema, kaburi, ningepata fasiri yake, ikisema, *"Jehanum." Jehanum* ni "kaburi." Kila wakati liliposema kuzimu," *Jehanum*, kaburi." Nami nikaliacha tu peke yake mpaka nilipopata nililokuwa nikinena habari zake, ndipo nikahubiri juu ya kuzimu; basi hata nilipopata hakika, picha nzima, na kuona mahali ilipokuwa. Kwa sababu, ninajisikia ya kwamba mhudumu anawajibika kwa Mungu, yale anayoliambia kusanyiko hilo, kwa sababu wao watashikilia kabisa jambo hilo. Na kwa hiyo, basi, vipi kama nitawafanya washikilie mahali pasipo sahihi, halafu wakati ufikie ambapo kushikilia huko hakutasimama? Mnaona?

Na katika ono lile alilonipa Bwana, wakati fulani uliopita, wakati mamilioni… wakati Yule aliyekuwa akinena nami, alisema, "Utahukumiwa wewe, kwanza, kwa Injili unayohubiri."

Nikasema, "Ninahubiri jambo lile lile alilohubiri Paulo, na hao wengine."

Na mamilioni hayo yote ya sauti yakalia kwa sauti kuu, "Tunatumainia jambo hilo." Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Mnaona? Sawa.

10 Kwa hiyo nataka kuendelea usiku wa leo, sasa, ili tusichukue muda mrefu sana. Na msisahau sasa … Sasa, asubuhi ya leo … Nina maandishi machache hapa. Asubuhi ya leo nilinena juu ya Danieli akiwa kifungoni, Gabrieli akimjia na kumpa maagizo ya wakati ujao. Hayo ndiyo tuliyokuwa nayo asubuhi ya leo, maagizo ya wakati ujao.

Sasa, usiku wa leo, tunazungumza juu ya Sababu Sita za Kusudi La Gabrieli Kumzuru Danieli. Jumapili ijayo, Bwana akipenda, kuyaweka hayo majuma sabini, mahali pake, katika ratiba ya wakati. Nasi tunasimama wapi? Sasa, kama tunaweza tu kupata jambo hilo na kulihakikisha, yakini, basi tutajua tu saa tunayoishi. Sasa, hatutajua Yeye atakuja lini; hakuna mtu atakayejua hilo. Yesu hajui jambo hilo, Yeye Mwenyewe. Yeye alisema hakufanya hivyo. Alisema ni Baba tu, pekee, aliyejua jambo hilo. Wala hata Malaika hawalijui. Hakuna mmoja wetu anayejua wakati Yeye atakapokuja, lakini tunaweza kujua ile—ile saa ambayo…wakati tunaoishi, kujua jinsi tu tunavyoweza kuwa tuko karibu.

11 Sasa, ili kurudia kwa kifupi, kwa sababu hao wavulana wananasa kanda za huu… Mitambo inafanya kazi kule nyuma kwenye kile chumba. Nazo kanda, bila shaka, zinatumwa, kila mahali.

Sasa, katika somo la asubuhi ya leo, baada ya kurudia kwa ufupi mlango wa 4 na wa 5, ndipo tulifikia…kuanzia mlango wa 9 wa Danieli. Na sasa, usiku wa leo, tunaendelea na sura ya 9. Kabla hatujaliendea, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo na kuzungumza na Mwandishi wa Neno.

12 Mungu wetu mwenye neema, tuna hakika ya kwamba unajua kusudi la moyo wetu. Unajua ni kwa nini tuko hapa. Nawe unajua ya kwamba hatukuja usiku wa leo kwa sababu tu tulifikiri ingekuwa ni mahali pazuri pa kuja, kupumzika kidogo kwa ajili ya alasiri. Baba, siamini kuna mtu mmoja aliyepo hapa aliye na kusudi hilo. Ninaamini ya kwamba tuko hapa usiku wa leo kwa sababu tunamaanisha kabisa, tunaamini, na tunataka kujua BWANA ASEMA HIVI.

Tunakupenda, Bwana, na tunapenda Neno Lako. Na kama mahali hapa ambapo umetuandalia, kuwa na dari tu juu ya vichwa vyetu, na kuta hizi za mawe, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya mahali hapa. Kwa kuwa, tunaamini ya kwamba kuna Makao ng'ambo ya mbingu, ambako tunaelekea. Nasi tunawawazia babu zetu ambao hata hawakuwa na majaliwa haya, na linatufanya tuinamishe mioyo yetu kwa aibu, Bwana, kwa kunung'unika.

Sasa, Baba, tunaomba ya kwamba utatufungulia, usiku wa leo, Maandiko. Njoo, tembea, karibu na

kila mmoja wetu, tunaposhuka kwenda barabarani usiku huu. Nena nasi kama ulivyofanya kwa wale waliokuwa wakienda Emau, kutoka Yerusalemu. Ili kwamba, wakati ibada itakapokwisha, usiku wa leo, huenda tukaenda kwenye nyumba zetu mbalimbali na kusema, "Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu tulipomsikia akinena kupitia Neno Lake!"

Bariki kusoma huku. Bariki jitihada zangu dhaifu, Bwana. Fungua kinywa changu kwa mambo yale yaliyo ya kweli, na ukifunge kwa yale yaliyo makosa. Na ujipatie utukufu Mwenyewe, na utukufu katika watu Wako, wapate kuona ile saa tunayoishi na kule kukaribia kwa Kuja kwa Bwana Yesu. Kwa kuwa, tunaomba katika Jina La—Lake, Jina la Yesu Kristo. Amina.

13 Sasa, ili kurudia kifupi Maandiko yetu kwa muda mfupi, tunaona ya kwamba Danieli alikuwa uhamishoni kwa muda mrefu wa miaka sitini na minane. Wazieni jambo hilo! Sasa, ninyi, na karatasi zenu na penseli, ambao hamkulipata asubuhi ya leo, mnaweza kulichukua tena usiku wa leo. Kutoka A.D. 606 hadi 538. Toa 538 kutoka 606, unapata miaka sitini na minane ambayo Danieli alikuwa katika…mateka; hana kanisa la kuhudhuria, hana mahubiri ya kusikiliza, hakuna cho chote. Lakini alikuwa na vitabu vichache, magombo machache, ambapo nabii aliyemtangulia alikuwa ametabiri, na huyo alikuwa ni—alikuwa ni Yeremia.

14 Sasa, wakati alipokuwa akiyasoma Maandiko, aliona wakati ulikuwa unakwisha, ule wakati wa ile miaka sabini… Naye Danieli aliamini kwa uchaji kila Neno ambalo nabii Yeremia alinena. Nami ninasema jambo hili, kwa darasa langu usiku wa leo: Je! tungepaswa kuwaamini manabii wetu? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Naam, bwana. Kwa kuwa, Neno la Bwana liliwajia manabii. Wao wana BWANA ASEMA HIVI. Na nabii wa kweli hatatofautiana kamwe na lile—lile neno la nabii mwingine. Kamwe hawatamfanya aseme jambo ambalo halisemi. Watasema yale hasa nabii wa kweli aliyosema. Hilo linawafanya kuwa nabii. Ndipo watakapopata jambo hilo, na halafu wanatabiri yale yatakayokuja, wakijua jambo hili, wakiwa na hofu moyoni mwao, wasije wakasema jambo baya na lingempoteza mtu fulani. Hatutaki kamwe kufanya hivyo. Tunataka kuwa na hakika kabisa ya kwamba tuna Neno la Bwana kabla hatujasema BWANA ASEMA HIVI. Mnaona? Haina budi kuwa ni ujumbe mkamilifu, wa moja kwa moja kutoka kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, la sivyo hatupaswi kamwe kuusema.

15 Sasa, wakati alipokuwa akisoma Maandiko, aliona ya kwamba ile miaka sabini ilikuwa ikiisha. Kwa hiyo, yeye akiwa amekaa kule miaka sitini na minane, ilikuwa imesalia miaka miwili ya wakati ujao kisha Mungu angewarudisha watu Wake kwenye nchi ya uenyeji wao.

Alipokuwa katika maombi, tunaona ya kwamba kulikuwa na Malaika mwenye nguvu aliyetoka Mbinguni. Kuna mtu anayeweza kutaja jina Lake? [Kusanyiko linasema, "Gabrieli." — Mh.] Gabrieli. Naye ni Malaika kwa kanisa la Kiyahudi. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Kila mahali, ni Gabrieli. Gabrieli ndiye mjumbe wa kanisa, kanisa la Kiyahudi; akamjia Mariamu; Alimjia Zakaria. Daima, ni Gabrieli. Naye ni mmoja wa Malaika wakuu wa Mbinguni. Na je! hakumletea Ndugu yetu Danieli salamu nzuri sana kutoka kwa Mungu! "Loo, Danieli, unapendwa sana!"

16 Je! hilo halingekufurahisha, kuwazia ya kwamba Mungu amekupenda? Kama nisingekuwa ninapendwa sana, ningetaka tu kujua ya kwamba kwa namna fulani ninapendwa kidogo kule Juu, nawe je? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hakika. Kwa namna fulani tu … Yeye ananiwazia, mara kwa mara, lingenifanya tu nitake kupaza sauti, kuwazia ya kwamba hata ananijali. Nasi tuna hakika ya kwamba anatushughulikia, kwa sababu, "Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa mahali petu," ndugu. Na, sasa, sisi ambao tulikuwa wageni kwa Mungu, sasa ametuleta karibu na Mungu na ametupa arabuni ya wokovu wetu, yaani, Roho Mtakatifu. Pamoja na imani humo ndani inayotuinua sisi juu ya mambo ya ulimwengu, nasi tunaenda juu ya hayo. Hilo ni jambo lenye fahari. Sivyo? ["Amina."] Vema.

17 Alipokuwa katika maombi, Gabrieli akaja na kumwambia ya kwamba hakukuwa tu na miaka miwili zaidi iliyosalia kabla hawajarudi kwenye nchi ya uenyeji wao, lakini alimwambia mwisho wa safari nzima ya taifa hilo. Wazia jambo hilo! Mwisho wa safari yote, kila safari ya duniani, Gabrieli aliielezea kwa Danieli. Kasema Yeye alitumwa amwambie Danieli jambo hili kubwa. Jinsi gani nabii huyo hapana budi alijisikia! Naye akamwambia ya kwamba kulikuweko na majuma sabini yaliyokusudiwa watu wale, mpaka mwisho wa yote; yaani wakati wa mwisho, kwa hiyo yote yamekwisha, ule mwisho. Yeye alisema, "Kuna majuma sabini."

Wengine wao wanayafanya hayo kuwa ni miezi, wengine siku, wengine… A-ha! Kama kweli ni majuma, kuna kama miaka miwili tu na robo, ama mwaka mmoja na robo wa hayo. Na, mnaona, ninyi … Hapo ndipo tunapaswa kupata, kuwa wakweli.

18 "Majuma sabini yamekusudiwa juu ya watu wako." Kwa kusudi gani? Kwa nini? Yalikusudiwa juu ya watu wa nani? Watu wa Danieli, Wayahudi. Na yamekusudiwa kwa sababu gani? Si juu ya Danieli peke yake, lakini juu ya mji mtakatifu wa Danieli; unaona, mji mtakatifu wa Danieli. Sasa, darasa, mji mtakatifu wa Danieli ulikuwa ni upi? [Kusanyiko linasema, "Yerusalemu." — Mh.] Yerusalemu.

Na sasa tutachukua, labda tutalifikia usiku wa leo: Yerusalemu ulikuwa wapi? Ni nani aliyeuanzisha

Yerusalemu? Je! Ulipata kuwazia jambo hilo? Ni nani aliyeuanzisha Yerusalemu? Ulianzishwa lini? Tutafikia jambo hilo, baada ya muda mfupi. Ni nani aliyeuanzisha Yerusalemu? Jamani, ni jambo dogo lililofichwa nyuma huko pembeni, lakini hakika Hilo linatuambia jambo hilo. Naam, bwana. Ni nani aliyeuanzisha Yerusalemu, nao ulianzishwa lini? Vema. Na huo ni mji mtakatifu wa Danieli.

19 Nasi tunafahamu ya kwamba mji ule, ambao sasa umekuwa laana kwa muda wa miaka elfu mbili, utajengwa upya na kuanzishwa tena. Na ibada ya hekaluni itaanzishwa kama tu ilivyokuwa hapo mwanzo. Hiyo ni kweli. Yerusalemu utakuwa hivyo, sikiliza, na kutakuwako na sadaka, dhabihu itatolewa tena kama tu ilivyokuwa hapo mwanzo. Tutayafikia karibu mambo hayo yote, nadhani, usiku wa leo, ama mengi ya hayo.

20 Sasa nawatakeni mjue, enyi marafiki, ya kwamba, ninapoyagusia mambo haya, bila shaka ninaacha majuma kadha ya mafundisho. Lakini kwa namna fulani nayagusia tu, ili kwamba wakati hali ya hewa itakapokuwa baridi kidogo, ama baadaye kidogo, tutakapoingilia hiyo Mihuri Saba, Vitasa Saba, Baragumu Saba, mambo haya yote, ambayo ninaweza kuyarejea na kusema, "Mnakumbuka yale majuma sabini ya Danieli? Mnakumbuka wakati wa Kanisa, wakati lilipopaa juu, na yale yaliyotukia?" Na majuma haya sabini ya Danieli yanachukua kutoka kupaa juu kwa Kanisa mpaka kurudi tena kwa Kanisa. Kipindi hicho ndicho yanachohusika nacho. Sasa, basi, si yale majuma yote ya Danieli; sehemu yake. "Majuma sabini yameamriwa."

21 Basi, kulikuweko na sababu sita za kusudi la kuzuru Kwake, kumwambia yale yatakayotukia. Sasa, kulikuweko na sababu sita za kusudi la kuja Kwake. Basi, usiku wa leo, nafikiri tutaachia hapa katika Maandiko ya mahali tulipokuwa asubuhi ya leo, ambapo kwamba palikuwepo na kusudi lenye sababu sita. Tuko hapa. Basi tunaona ya kwama kulikuwa na kusudi sita, moja yake. Sasa hebu na tuchukue mlango wa nne… kifungu cha nne…24 cha mlango wa 9 wa Danieli.

*Na muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako, …*

Sasa kumbukeni, hiyo ndiyo ile safari yote ya Israeli watayokuwa nayo duniani. Yameamriwa. Majuma sabini yameamriwa tu. Hayo ndiyo tu waliyopewa Wayahudi.

*…juu ya watu wako, na juu ya mji wako mtakatifu,..*

Kwa hiyo, majuma haya sabini, sasa msilikose, yatafunua tangu wakati huo mpaka mwisho wa Wayahudi, na pia mpaka mwisho wa Yerusalemu, mpaka utakapojengwa mji mpya. Sasa, loo, natumaini tutaingilia jambo hilo, vizuri sana na katika kilindi.

*…umeamriwa juu ya watu wako, na juu ya mji wako mtakatifu,…(Kufanya nini?)…ili kukomesha makosa,…*

22 Yeye alimwambia nini sasa? Alikuwa akijaribu kujua itachukua muda gani. "Ninajua tuko katika wakati wa mwisho." Kama tulivyo sasa, "Bwana …"

Ni wangapi kwenye darasa hili, usiku wa leo, wanaoamini ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho? Sema, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Asanteni. Tuko mwishoni. Sasa tunajaribu kuona, kutoka kwa Mungu, kwamba jambo hilo litachukua muda gani. Tunaishi siku gani? Hiyo ndiyo sababu tunarudi nyuma na kuchukua manabii hawa, na kadhalika, na kujaribu kupata mahali tulipo.

23 Na hivyo ndivyo Danieli alivyofanya. Aliuelekeza uso wake kwa Mungu. Ni wangapi waliosoma Danieli 9 leo, inueni mikono yenu. Vema. Mnaona maombi yake, jinsi alivyotubu kwa ajili ya watu wake, na toba yake mwenyewe. Alitaka kuwa na hakika ya kwamba alijua walikuwa wanarudi lini, kwa sababu alitaka kuwaweka watu tayari kurudi.

Sasa, ninalojaribu kufanya, ni kupata kujua tunapaa juu lini, na kuwatayarisha watu kupaa juu, waliokuwa tayari. Nasi tumeuelekeza uso wetu kwa Mungu, katika maombi na kusihi, kupata kujua, "Bwana, tunaishi katika saa ipi?"

24 Tumeona mambo yote haya mbalimbali yakitendeka; tunaona ulimwengu ukiwa katika machafuko. Tunaona wakati umewadia. Yale ninii…maandishi ya mkono yako ukutani, kila alichosema Mungu. Tunamsikia Rais wetu akizungumzia juu ya vita vingine, vinavyokuja hivi sasa. Tunasikia ubashiri, "Katika, loo, katika masaa machache baada ya vita, imebashiriwa ya kwamba mataifa hayatakuwa kitu ila mavumbi ya volkeno." Nasi tunajua limetupata.

Kwa hiyo tunajua, kabla jambo hilo halijatukia, Kanisa halina budi kuondoka. Kwa hiyo, "Bwana, tuko wapi?" Hiyo ndiyo sababu ninaamini ya kwamba Yeye atatuому kujua. Tunaelekeza nyuso zetu kujua. Sasa, kwanza, hebu tuone.

*Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako,…mji wako mtakatifu, kukomesha makosa, …kuishiliza dhambi, na kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu,…kuleta haki ya milele, …kutia muhuri maono na unabii, na kumtia mafuta yeye aliye Mtakatifu sana.*

Hizo ndizo sababu sita za kusudi la kuzuru kwa Gabrieli.

25 Sasa hebu tuanze, namba moja. Kama mkitaka kuliandika, ninyi mlio na penseli. Namba moja, "Kukomesha makosa," hilo ndilo jambo la kwanza. Sasa, kukomesha makosa ya Israeli, ambao walimkosea Mungu, kutakuwa ni kuondoa maovu ya Yakobo.

Sasa, kupata jambo hili, hebu na tufungue Warumi. Mlango wa 11 wa Warumi, na tuanzie na kifungu cha 21 cha Warumi 11. Sasa tutafanya nini? "Kukomesha makosa." Warumi 11:21. Vema.

> *Kwa maana ikiwa Mungu hakuyaachia tawi la asili,* … (Ambalo lilikuwa ni nani? Israeli.) ... *angalia…wala hatakuachia wewe.*

Sasa, ninawatakeni, mtakapoenda nyumbani, msome kifungu hiki chote cha 11. Ninasoma tu hiki ili… Andikeni mlango wote wa 11, na mkausome.

> *…hatakuachia wewe.*

> *Tazama, basi, wema…ukali wa Mungu; kwa wale walioanguka,…bali kwako wewe wema wa Mungu, ukikaa katika wema huo; kama sivyo, wewe… utakatiliwa mbali, nawe utakatiliwa mbali.*

> *Na hao pia, wasipokaa katika kuto-…wasipokaa katika kutokuamini kwao, watapandikizwa; kwa kuwa Mungu aweza kuwapandikiza tena.*

Mnaona, akiwaambia ya kwamba kutakuweko na wakati ambapo kwamba Mataifa watakatiliwa mbali, na Israeli warudi tena.

> *Kwa maana ikiwa wewe ulikatwa ukatolewa katika …katika mzeituni, ulio mzeituni mwitu kwa asili yake*, (Mataifa), *kisha ukapandikizwa, kinyume cha asili,…*

Tulikuwa kinyume cha asili, wageni, bila rehema, bila Mungu, bila tumaini lo lote. Naye Mungu, kwa rehema Zake, apate kutupa nafasi, aliwakatilia mbali Israeli wenye haki kwa sababu ya makosa yao, na kuwaweka kando, ule…ule mzeituni ulio mwema, na akaingiza mzeituni mwitu, kinyume cha asili.

> *…katika mzeituni ulio mwema; si zaidi sana wale walio wa asili kuweza kupandikizwa katika mzeituni wao wenyewe?*

Vema, hebu na tuendelee kusoma.

> *Kwa maana, ndugu zangu, sipendi msiijue siri hii, ili msijione kuwa wenye akili; ya kwamba kwa sehemu ugumu umewapata Israeli, umewapata Israeli, mpaka utimilifu wa Mataifa ... uwasili.*

26 Mpaka Mungu atakapomaliza na Mataifa, Israeli walipofusha. Waliingia katika dhambi na kumkosea Mungu, kwa sababu Mungu aliyapofusha macho yao, tupate kupandikizwa. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Kifungu cha 26 sasa.

> *Na hivyo Israeli wote wataokoka;…*

Mungu aliwapofusha makusudi kwa ajili yangu na yako. Hawawezi kuona, kwa sababu Mungu aliwapofusha. Na Israeli wote, Israeli wa kweli, wataokolewa. Malaika alisema nini? Utukufu! "Kukomesha makosa ya Israeli! Nimekuja kukwambia ya kwamba wakati unakuja wakati makosa ya Israeli yatakomeshwa." Mungu atakatilia mbali tawi hilo mwitu, na kulipandikiza kwenye huo, kulirudisha, tawi hilo halisi tena.

Loo, wakati mwingine linaufanya moyo wangu uruke, kuwaona maskini hao watu, wenye mashaka waliokatiliwa mbali huko, bila kujua wanakoelekea; na ninafikiri ya kwamba Mungu, katika rehema Zake, alifanya jambo hilo ili kwamba nipate kuokolewa. Akayapofusha macho yao wasimjue Masihi wao wenyewe, akayafumba masikio yao kwamba hawakuweza kumsikia Yeye; hata hivyo, waliitazama moja kwa moja miujiza Yake, na waliitazama moja kwa moja kwa miujiza Yake na mambo aliyokuwa anafanya.

27 Mathayo, ninaamini, mlango wa 12, ama wa 8 ama mlango wa 12, ilisema, "Ingawa Yesu alifanya miujiza mingi namna hiyo, hawakuweza kuamini." Kwa sababu, Mungu alisema, "Wana macho nao hawawezi kuona, na masikio nao hawawezi kusikia; wasije wakaona kwa macho yao na kusikia kwa masikio yao, nami ningewaokoa." Lakini, ili kwamba tuweze kupata nafasi, Yeye alivuta pazia juu ya macho ya watoto Wake Mwenyewe, akawafukuza watoto Wake mwenyewe kutoka mezani, na akawafukuza wakonde katika mambo ya Roho, kusudi apate…tupate nafasi ya kuishi, akitupa Uzima. Kifungu cha 26, tena.

> *Na hivyo Israeli wote wataokoka; kama ilivyoandikwa. Mwokozi atakuja kutoka Sayuni; atamtenga Yakobo na maasi yake.*

Naam, Yeye atakuja kwenye Mlima Sayuni, moja ya siku hizi. Wao watamtambua Yeye, juu ya Mlima wa Mizeituni, na Israeli wote watajua ni Yeye. Mataifa watakuwa wamekwisha wakati huo. Hilo tawi lililopandikizwa, Mungu atatoa kwake matunda yaliyokusanywa. Na tawi hilo la mwitu litakuwa …

28 Na sasa kumbukeni, hapa nyuma mnaposoma, Yeye alisema, "Kama hayo mashina yalikuwa matakatifu, na hayo mashina yalikuwa Shina takatifu, kadhalika na matunda yanayotoka kwenye Shina hilo takatifu yataleta matunda matakatifu." Na kama Shina hilo lilikuwa ni Yesu Kristo, Ambaye ni Shina na Mzao wa Daudi pia; kama Uhai huo uliokuwa ndani Yake, ulipitia katika kizazi cha Wayahudi na ukakatiliwa mbali toka kwa watu, na macho yao yakapofushwa tupate kuona, maisha yetu yatapaswa kulingana na Tawi hilo lililobarikiwa. Loo, naam, ndugu. Hiyo ni kweli.

29 Mungu aliwakatilia mbali, makusudi, na kupofusha macho yao kusudi tupate nafasi ya kuona, akitupa sisi nafasi. Nasi tunatembea kila mahali kana kwamba sisi ni watu wakuu. Paulo anawaambia hapa, "Angalieni, jinsi mnavyotenda jambo hilo. Angalieni! Kwa maana ikiwa Mungu hakuliachilia tawi la asili, Yeye atakuwaje na rehema tena kwa tawi mwitu ambalo tayari…"

Kwa hiyo tunatembea hapa na pale, kusema, "Mimi ni Mpresbiteri! Mimi ni Mmethodisti! Mimi ni Mbatisti! Mimi ni Mpentekoste!" Hilo halimaanishi kitu kwa Mungu. Huna budi kuzaliwa mara ya pili kwa huyo Roho Mtakatifu anayetoka kwenye Shina. Lakini Yeye alikuja …

Sasa, kumbukeni, Yeye hasemi juu ya Mataifa. Ninalitupia tu jambo hili ndani hapa kusudi mwone nafasi ya Mataifa ilipo.

30 Lakini, Yeye alikuja "kukomesha makosa," kuyamaliza. Sasa, kama tukirudi nyuma katika Danieli tena, nasi tutaona ya kwamba katika Danieli, tunaona hapa, kifungu cha 24. Vema. "Kukomesha makosa." Kukomesha nini? Kukomesha makosa ya Israeli.

*Kukosea* ni nini? Ni kufanya kinyume cha jambo fulani. Kunikosea, ni kunitendea vibaya. Kukukosea, ni kukutendea vibaya.

Kwa hiyo, Israeli walimkosea Mungu. Na katika juma hili la sabini, kutatukia nini? Mungu atakomesha makosa ya Israeli. "Kukomesha makosa," kutakuwa ni, "kumwondolea Yakobo maasi yake." Na ndipo Israeli wote watazaliwa mara ya pili. Wote watampokea Roho Mtakatifu.

Sasa, namba mbili, andika hayo kwenye karatasi yako.

31 Tungeweza kudumu muda mrefu juu ya jambo hilo, lakini sitaki kuanza kuhubiri juu ya jambo hilo. Ninataka tu kuzungumza nanyi, ili kwamba mpate kulifahamu vizuri. Tutakapoifikia hii Mihuri Saba, basi mtaenda moja kwa moja mpitie lile Kanisa, mpitie ile Mihuri, mpitie yale Mapigo, na mjue mahali tunaposimama. Vema.

Namba mbili, "Kuishiliza dhambi." Sasa hebu tusome tena, Danieli.

> *…kukomesha…makosa, na—na kuishiliza dhambi,…*

Hilo ndilo kusudi lake la pili la kuja. Kwanza, ni kukomesha makosa ya Israeli; na kuishiliza dhambi. Israeli walitenda dhambi wapi? Walitenda dhambi yao kubwa wapi? Ni wapi walipojitenga na Mungu?

32 Sasa sikilizeni kwa makini. Hebu tufungue Mathayo Mtakatifu 24. Na hapa ndipo Israeli walipofanya kosa lao la kufisha. Hapa ndipo walipotenda dhambi yao ya mwisho, na sababu ya wao kuwa katika hali waliyo nayo siku hizi. Mathayo, mlango wa 27 wa Injili ya Mathayo Mtakatifu, na kifungu cha 25 cha sura ya 27. Hebu tuanzie kwenye—kwenye kifungu cha 21.

> *Basi liwali akajibu, akawaambia, Mnataka niwafungulie yupi katika hawa wawili? Nao wakasema, Baraba.*

Sasa kumbukeni, hiyo ni Israeli. "Baraba!"

> *Pilato akawaambia, Basi, nimtende-…nimtendeje Yesu aitwaye Kristo?* (Wasikilizeni!) *Wakasema wote, Asulibiwe.*

Kumbukeni, huyo ni Masihi wao ambaye Danieli alisema angekuja. Mnakumbuka katika somo la asubuni ya leo hapa, "Atakatiliwa mbali, si kwa ajili Yake," si kwa jambo lo lote alilofanya.

> *… Aasulubiwe.*

> *Ndipo liwali akasema, Kwani? ni ubaya gani alioutenda? Wakazidi sana kupiga kelele, wakisema, Na asulibiwe.*

> *Basi Pilato alipoona ya kuwa hafai lo lote, bali ghasia inazidi tu, akatwaa maji, akanawa mikono yake mbele ya mkutano, akasema, Mimi sina hatia katika damu ya mtu huyu*

*mwenye haki; yaangalieni haya ninyi wenyewe.*

Sikilizeni! Hili hapa kosa lao. Hii hapa dhambi yao.

*Watu…wakajibu, Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu.*

33 Hapo ndipo walipoitenda. Yeye alikuwa akiishiliza dhambi kwa ajili yao. Yeye angefanya jambo lipi lingine ila kuwasamehe, akijua ya kwamba ilimbidi kuyapofusha macho yao, ili tupate kuingia. Ni kama watoto Wake mwenyewe kulilia Damu Yake. Nao walipofushwa, Naye alijua walikuwa wamepofushwa. Hiyo ndiyo sababu aliwalilia wapate msamaha. "Wasamehe, Baba, kwani hawajui walitendalo." Walikuwa vipofu. Kwa ajili yetu walifanywa vipofu. Katika kutokuamini kwao walifanya jambo hili. Lakini watakapomwona tena … Amina!

34 "Kuishiliza dhambi." Dhambi ni nini? Kutokuamini. Hawakuamini huyo alikuwa ni Masihi. Hawakuweza kumwona kwamba ni Masihi, ingawa alifanya kila ishara aliyopaswa kufanya Masihi. Lakini hakuweza kuona jambo hilo. Walikuwa vipofu.

Kwa hiyo unapowaona watu wakisema, "Siamini katika kuponya Kiungu. Siwezi kuona jambo hilo. Siwezi kuona jambo hili la ubatizo wa Roho Mtakatifu." Usiwakasirikie; wao ni vipofu. Wanasema, "Siwezi kuona Ujumbe huu wa Kuja Kwake. Siwezi kuona huu ubatizo wa Roho Mtakatifu. Siwezi kuona uzao wa nyoka. Siwezi kuona jambo hili." Wao ni vipofu, wala hawajui. Waombeeni tu. Vema.

35 Katika kutokuamini kwao; lakini, watakapomwona, wakati Yeye atakapokuja tena, kutaishiliza kutokuamini kwao. Loo, jamani! Hebu tufungueni tu kwanza katika Mwanzo 25, mlango wa 45, na tupate m—mfano wa jambo hilo. Nimeandika hapa machache, Mwanzo wa 45, ninyi mnaoandika mihtasari. Loo, jinsi ninavyoipenda Injili hii nzuri ya kale! Vema. Sasa tunajua mahali tulipo.

Mnaweza kunisikia vizuri, huko nyuma ya jengo? Inua mkono wako kama unaweza kunisikia. Nimeiweka hii karibu kidogo.

36 Sasa tutasoma sehemu ya Maandiko haya. Ninawatakeni msikilize, ninyi ambao hamna Biblia yenu. Ninyi mlio na Biblia yenu, ni Mwanzo. Kwanza, hebu tuanzie katika mlango wa 44, kuanzia kifungu cha 27.

Ni Yusufu, naye Yusufu alikuwa ni mfano mkamilifu wa Kristo. Tunajua jambo hilo. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Alichukiwa na ndugu zake (kwa nini?) kwa sababu alikuwa wa kiroho, aliona maono, alifasiri ndoto. Yeye alikuwa mtu wa kiroho miongoni mwa ndugu zake, nao walimchukia. Naye baba yake alimpenda.

Vivyo hivyo Yesu alichukiwa na makanisa ya kimadhehebu, bali alipendwa na Baba Yake Mungu. Kwa nini walimchukia? Kwa sababu Yeye alikuwa wa kiroho. Kwa sababu … Walimwambia, walisema, "Yeye alikuwa mpiga ramli, pepo."

37 Mnakumbuka vile ndugu zake Yusufu walivyomwambia? "Huyu hapa yule mwotaji anakuja." Mnaona? Mnaona, jambo lile lile. Nao walimwuza Yusufu kwa karibu bei ile ile Yuda aliyomwuza nayo Yesu, vipande thelathini vya fedha. [Ndugu Branham alipiga mimbara mara kadha — Mh.] Wakamtupa katika shimo, kisha wakaenda wakamwambia baba yake ya kwamba aliuawa na kitu fulani, alikuwa amekufa. Lakini alitolewa kutoka kwenye shimo hilo. Kristo alitupwa shimoni, kisha akatolewa mle. Na kutoka hapo alienda hata mahali pa juu sana palipokuwepo duniani. Amina! Yusufu alienda mkono wa kuume wa Farao; naye Yesu akaenda kwenye mkono wa kuume wa Mungu. Katika kujaribiwa kwake, kabla ya kutukuzwa kwake. Yesu, kabla hajatukuzwa, alipitia majaribuni.

38 Mbona, ninaamini ilikuwa Billy Sunday, yule mwinjilisti mashuhuri, aliyesema, "Kila—kila mti ulikuwa na Malaika milioni moja wameketi juu yake, siku hiyo ya kusulibishwa, kasema, 'Vuta utoe mkono wako utuelekezee. Tutabadilisha hali ya mambo hapa.'" Bali asingeweza kufanya hivyo.

Kayafa akasema, "Alijiokoa mwenyewe; wengine hawezi kuwaokoa." Yeye hakujua alikuwa akimpa sifa. Kama angalijiokoa Mwenyewe, hangeweza kuwaokoa wengine. Kwa hiyo, Yeye alijitoa Mwenyewe, apate kuwaokoa wengine. Mnaona, vipofu sana kwa jambo hilo. Sasa wao …

39 Ndipo wakati alipokuwa pale katika kutukuzwa kwake, ama kabla ya kutukuzwa kwake, ama kujaribiwa kwake. Kumbuka, Yusufu aliwekwa gerezani kwa sababu hakuwa na hatia. Warumi, ama …

Yule jemadari Mwisraeli, jina lake Potifa; Potifa alienda, na akaenda safarini. Alikuwa na mke mwenye sura nzuri, naye mke wake akamwita Yusufu aje aingie ndani ya nyumba afanye jambo fulani; naye alijaribu kumfanya Yusufu afanye jambo baya akosee. Naye alikuwa mwaminifu kwa Mungu. Nawaambia, wao daima …

40 Ninyi wanawake, nimewakemea; sasa nitawatetea, kwa muda kidogo. Mnaona? Mwanamke ndiye chombo dhaifu zaidi. Ninajua hapawezi kuwa na mwanamume mbaya kabla ya mwanamke mbaya. Lakini mwanamume anayejua jambo hilo, wanaume wanaojua ya kwamba wewe ni mwana wa Mungu, na kufaidi

udhaifu wa mwanamke, unatia aibu; hata afanye nini. Yeye ni chombo dhaifu zaidi, nanyi mnajua jambo hilo. Kama yeye akitoka, akitenda isivyompasa mwanamke wa heshima, mshike mkono uzungumze naye kama dada. Wewe ni mwana wa Mungu. Usifanye mambo hayo maovu. Mwangalie Yusufu, alikuwa ni mfano kwako.

41 Na wakati mke wa Potifa, huyu mwanamke mrembo, wa kuheshimika, wa cheo cha juu sana, mmoja wa wanawake wenye cheo cha juu sana nchini, alipomsihi na kumshawishi. Ndipo akageuka, na huyo mwanamke akamshika na kujaribu kumkumbatia kwake. Naye akajivuta ghafla mpaka hata koti lake likamvuka, akamkimbia. Naam, bwana. Ndipo alipokuja, wakasema uongo juu yake, wakasema alikuja kumshika kwa nguvu, naye akaacha ninii yake…naye akaacha koti lake pale. Na kwa ajili ya jambo hilo akaenda gerezani. Lakini, kule gerezani, Mungu alikuwa pamoja naye, haidhuru walimweka wapi.

Yeye alikuwa ni mfano wa Mwana wa ufanisi. Kila kitu alichofanya Yusufu kilifanikiwa. Na wakati Yesu atakaporudi katika ule Utawala wa Miaka Elfu, hiyo ndiyo sababu majangwa yatachanua kama waridi. Kila kitu afanyacho kitafanikiwa. Yeye ni Mwana wa ufanisi. Po pote ulipomweka Yusufu, palibarikiwa. Popote alipo Yesu, pamebarikiwa. Kwa hiyo, mwingize moyoni mwako upate kubarikiwa.

42 Kwa hiyo tunaona sasa, ya kwamba, Yusufu basi aliwekwa gerezani. Na huko gerezani kulikuweko na watu wawili; mmoja alipotea, na mmoja wao aliokolewa. Yesu, katika jaribio Lake msalabani, mwizi mmoja alipotea na huyo mwingine akaokolewa.

Wakati alipotukuzwa, Yeye alienda mkono wa kuume wa Mungu. Wakati Yusufu alipotukuzwa, alienda mkono wa kuume wa Farao, wala hakuna mtu angeweza kusema na Farao bila kusema na Yusufu kwanza na kupata ruhusa.

Na wakati Yusufu alipoondoka kwenye jumba la mfalme … Loo, jamani! [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja — Mh.] Wakati Yusufu alipoondoka kwenye jumba la mfalme, tarumbeta zililia, na watu wakakimbia mbele yake, wakisema, "Piga magoti! Yusufu yuaja!" Amina!

Na wakati Yesu atakapouacha mkono wa kuume wa Ukuu juu, baragumu zitalia. Na kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri, "Yesu Anakuja!" Hakika! Lakini kama …

Na, kumbukeni, wakati alipokataliwa na ndugu zake, alifanya nini? Alichukua mke Mmataifa; alichukua mke wa Kimisri. Wakati Yesu alipokatiliwa mbali kutoka kwa ndugu Zake kule nyuma, wale Wayahudi, Yeye alioa Bibi-arusi Mmataifa. Lakini sasa, baada ya miaka mingi, baada ya watoto kuzaliwa, Efraimu na Manase, yeye alikuwa na familia.

43 Ndipo, siku moja, ndugu zake wakaja kumtembelea. Angalia. Tunajua hadithi hiyo, jinsi alivyoweka jambo hilo dogo mle ndani, kurudisha. Na kujifanya kana kwamba hata hakuweza kuzungumza lugha yao; alikuwa na mkalimani, kufasiri Kiebrania, wakati yeye mwenyewe alikuwa Mwebrania. Na ndugu yao alikuwa ameshuka akaja. Hawakumjua. Alikuwa mtawala mkuu.

Na sasa hivi, Kristo anawazuru Wayahudi, anawaponya wagonjwa wao na kadhalika, na bado hawajui Yeye ni Nani, huyo Masihi.

Hebu tuanzie kwenye kifungu cha 27 cha mlango wa 44.

> *Mtumwa wako, baba yangu, akatuambia, Mnajua ya kuwa mke wangu alinizalia—mke wangu alinizalia wana wawili;*
>
> *Mmoja alitoka kwangu,…*

Huyo alikuwa ni Yusufu, yule yule waliyekuwa wanazungumza naye.

> *…nikasema, Bila shaka ameraruliwa, wala sikumwona tangu hapo.*
>
> *Na mkiniondolea huyu naye, na madhara yakimpata, mtashusha mvi zangu na msiba kaburini.*

44 Wao walikuwa na Benyamini mdogo kule chini, ndugu yake mdogo. Mnajua Benyamini anamwakilisha nani? Hili kundi jipya la Wayahudi halisi wanaokusanyika kule sasa kufanyiza hao mia na arobaini na nne elfu, taifa hili—hili linalokuja. Si kundi hili la wahuni wa Wall Street, la, la; hao ni chakula zaidi cha mzinga. Hao si Wayahudi. Hao si Wayahudi. Halisi ni hawa Benyamini wadogo wanaokuja kutoka chini huku, wala hawajapata kamwe kusikia Neno la Yesu Kristo.

> *Basi sasa, njoni kwangu … na baba yako … na baba yangu, wala mtoto hayuko pamoja nasi; akiona ya kwamba maisha yake yamefungwa katika maisha ya kijana;*

45 Maisha ya Mungu mwenyewe yameshikamana na ya Israeli. Yeye amemwoa. Tutalifikia hilo katika dakika chache, Bwana akipenda. Yeye amemwoa Israeli. Maisha yake yameshikamana naye. Kama tu vile mimi nilivyoshikana na Bibi Branham kule nyuma, mke wangu, nawe umeshikamana na mke wako. Maisha

yako yameshikamana na jambo hilo. Na Mungu amemwoa Israeli. Na ilikuwa ni kitu gani? Yakobo alisema, "Maisha yangu yameshikamana na ya mtoto huyu. Nitaninii …"

*Na itakuwa atakapoona ya kwamba huyu kijana hayuko, pamoja nasi, ...*

Yusufu alikuwa anataka kubaki na huyo mtoto, mwajua. Tunajua hadithi hiyo.

*…Na kwamba atakufa; baba yake, na watumwa wako, watashusha mvi za mtumwa wako, baba yetu, kwa huzuni kaburini.*

Sikilizeni ombi hilo ambalo Reubeni anatoa sasa.

*Kwa maana mtumwa wako alijifanya anamdhamini kwamba huyu kijana kwa baba ya-… kwa baba yangu, nikisema, nisipomrudisha…nisipomrudisha kwako, basi nitakuwa na hatia kwa baba yangu sikuzote.*

*Basi, sasa nakusihi, uniache mimi mtumwa wako nikae badala ya huyu kijana…*

Loo, jamani! Mnaona, anasimama moja kwa moja mbele ya Yusufu, ndugu yake. Huyu ni Yusufu, naye hamjui. Loo, ngoja mpaka huo Utawala wa Miaka Elfu utakapoanza, ndugu!

*…sasa badala ya huyu kijana kuwa mtumwa wa bwana wangu;…*

Msikieni, akimkiri yeye, kwamba ni "bwana."

... *na huyu kijana umwache aende pamoja na nduguze.*

*Kwa maana nitawezaje kumwendea baba yangu, na huyu kijana hayuko pamoja nami? Nisije nikayaona mabaya yatakayompata baba yangu.*

46 Akisihi, akitoa uhai wake mwenyewe! Jinsi hao Wayahudi watakavyosimama kule wameinua mikono yao! Angalia. Angalieni sasa kifungu cha 45, kifungu … Sikilizeni kwa makini, msilikose. "Wakati Yusufu alipoweza …"

*Hapo Yusufu hakuweza…-jizuia—kujizuia mbele yao wote waliosimama karibu naye…*

Ndugu, hapo ndipo dhambi itakapoishilizwa. Kutokuamini kutatawanyishwa.

... *Kisha akapiga makelele, akasema, Mwondoeni kila mtu mbele yangu. Wala hakusimama mtu pamoja naye, Yusufu alipojitambulisha kwa nduguze.*

Ni kitu gani? Hata mke wake mwenyewe alirudi kwenye jumba la mfalme. Loo, jamani! Bibi-arusi Utukufuni, Yesu atakaporudi (tutaingilia jambo hilo hapa) kujitambulisha.

*Akalia kwa sauti kuu …*

Yusufu hakuweza tu kujizuia tena, naye akapaza sauti akalia.

*…nao Wamisri wakasikia. Watu wa nyumba ya Farao wakasikia.*

47 Moja kwa moja mpaka kwenye jumba la mfalme, walimsikia Yusufu akipiga mayowe. Sasa, huo ulikuwa ni mfano wa Kristo akikutana na Wayahudi, ambapo, Yeye alijua aliwapofusha ili kwamba tupate nafasi. Lakini atakapokuja kwao tena, dhambi ya Israeli itakuwa imekwisha.

*Yusufu akawaambia ndugu zake, Mimi ndimi Yusufu;…*

Unafikiri Yesu atasema nini? "Mimi ndimi Masihi wenu. Mimi ndimi mliyemsulibisha."

*…baba yangu angali hai bado? Wala ndugu zake hawakuweza kumjibu, maana waliingiwa na hofu mbele yake.*

48 Loo, sina budi kusimama hapa kwa dakika moja. Hebu na tufungue Zekaria sura ya 12. Fungueni pamoja nami sasa kwenye Kitabu cha Zekaria, mlango wa 12 wa Zekaria. Na labda ninachukua kidogo muda mwingi sana katika kuanza kuhubiri juu ya jambo hili, lakini na—natumaini siyo. Na mimi—nami nataka mlipate, natamani mno.

Zekaria, hebu tufungue sura ya 12 ya Zekaria, na tuone atakayosema sasa wakati atakaposimama mbele ya ndugu Zake. Zekaria 12, na 10. "Kuishiliza dhambi," sasa. Vema, sura ya 12 na aya ya 10.

49 Angalia. Na sasa anazungumza hapa juu ya wale masalia; kule kuzingirwa kwa Yerusalemu; yule mnyama na yale majeshi vimeondolewa, na kadhalika; mambo yote yamefikia mwisho sasa; hii ni karibu kufikia ule Utawala wa Miaka Elfu, ule Utawala wa Miaka Elfu uko karibu kuanza sasa hivi.

*Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya*

(kitu gani?) *neema…*

Amina! Neema ya ajabu!

> *…watu wa nyumba ya…uenyeji wa Yerusalemu*, ("mji mtakatifu" wa Danieli) *roho ya* (kitu gani?) *neema na kuomba; nao watanitazama mimi ambaye waliyechoma; nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee; nao wataona uchungu kwa ajili yake, kama vile mtu aoneavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza.*

50 Sikilizeni, hayo yatakuwa ni maombolezo ya jinsi gani wakati yeye atakapokuwa amesimama pale, akijitambulisha kwao, kama alivyofanya Yusufu! Sikilizeni.

> *Siku hiyo kutakuwa na maombolezo makuu sana huko Yerusalemu, kama maombolezo ya Hadad…*

Siwezi kutamka jina hilo, H-a-d-a-d-r-i-m-o-…

> *…Hadadrimoni katika ... bonde la Megido—Megido.*

> *Nayo nchi itaomboleza, kila jamaa peke yake; jamaa ya nyumba ya Daudi peke yao, na wake zao peke yao; na jamaa ya nyumba ya Nathani peke yao, na wake zao peke yao;*

> *Ile ... Jamaa ya nyumba ya Lawi…na wake zao peke yao; na Simioni na zao peke yao.*

> *Jamaa zote zilizosalia, kila jamaa peke yake ... na wake zao peke yao.*

Wataona aibu sana, watakaposimama pale na kuona ya kwamba Mtu yule yule waliyemsulibisha na kumkana, amesimama pale, Yusufu wao mpendwa. Kutakuweko na maombolezo makuu sana! Nao watasema, "Je! ulipata wapi jeraha hizo?"

Yeye alisema, "Katika nyumba ya rafiki Zangu." Mnaona ninalomaanisha? Kuishiliza dhambi, ya kutokuamini, hilo ndilo Yeye analokuja kufanya.

51 Na mwaka huu wa sabini wa Danieli, juma la sabini, hasa, anakuja kuishiliza dhambi, kuiondoa. Mnaelewa sasa? Wa kwanza ni nini? "Kukomesha makosa." "Kuishiliza dhambi." Namba tatu, "Kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu." Ninyi ambao mnaliandika.

Nilikuwa na kama Maandiko mengine sita hapo, lakini ninayaruka tu, kwa sababu kuna joto. Hatutaki kuchukua wakati mwingi sana. Ninataka kufikia mengi ya jambo hili kadiri niwezayo, lakini bila kuwaweka kwa muda mrefu sana. Vema.

52 "Kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu." *Uovu* ni "kufanya makosa," kama walivyofanya pale msalabani. Yeye alifanya upatanisho, lakini hautawafaa wao. Haukuwafaa wao. Kwa nini? Kwa sababu wao walipofushwa na hawakuweza kuuona. Na kwa nini walipofuka?

Mnasema, "Vema, labda, leo…kwa sababu mimi ni kipofu." Wewe ni kipofu makusudi. Walikuwa vipofu kwa sababu Mungu aliwapofusha. Lakini wewe ni kipofu kwa sababu wewe ni kipofu makusudi. Hakuna upatanisho kwa ajili yako. "Msipoamini ya kwamba Mimi Ndiye," Yesu alisema, "mtakufa katika dhambi zenu." Hiyo ni kweli.

53 Sasa hebu na turudi kwenye Zekaria tena, mlango wa 13. Sasa hebu na tusikilize hapa. "Fanyeni upatanisho." Sasa, ambapo hii … Nilikuwa nikimtafuta mtu fulani, asikie hili—asikie hili, lakini labda Bwana atamfikishia kwa njia fulani.

> *Katika siku hiyo watu…*

"Katika siku hiyo." Dk. Scofield ameandika hapa chini pambizoni, ama kwenye kichwa chake cha kifungu cha lake, "Mabaki… Mabaki waliotubu wakielekeza msalabani."

"Kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu." Uovu, ni jambo ambalo umekosea, ambalo unalijua vizuri zaidi, ya kwamba hukupaswa kulitenda. "Kama nikiwaza maovu moyoni mwangu, Mungu hatanisikia."

54 Sasa, katika Zekaria mlango wa 13, hebu tuanzie ya kwanza, kwenye kifungu cha kwanza.

> *Katika siku hiyo watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, watafunguliwa chemchemi kwa dhambi na…unajisi.*

Kutakuwa na nyumba iliyofunguliwa. Endelea mbele; tungeweza tu kuendelea kulisoma. Ninataka ninyi mliandike ili mkasome. Lakini sasa, nimeandika hapa nianzie kwenye kifungu cha 6 na kusoma hata cha 10. Vema, hebu na tusome sasa na tuone, tusome hadi cha 9, hasa.

*Na mtu atamwambia, kwamba wapi…jeraha hizi ulizo nazo katika mkono wako ni nini? Naye atajibu, Ni jeraha nilizotiwa*…(Hebu tuone.)… *atajibu, …jeraha nilizotiwa katika nyumba ya rafiki zangu.*

*Amka, Ee upanga, juu ya mchungaji wangu, na juu ya mtu aliye mwenzangu, asema BWANA wa majeshi; mpige mchungaji, nao kondoo watatawanyika; nami nitaugeuza mkono wangu juu ya wadogo.*

55 Sasa, Yesu alinukuu Andiko hilo. Mnaona, "Mpige Mchungaji, na kuwatawanya kondoo." Lakini angalia katika kifungu kinachofuata. Yeye alinukuu tu kiasi hicho. Lakini angalia ile sentensi yake inayofuata inavyosema, sehemu yake inayofuata. "Nami nitaugeuza mkono wangu juu ya wadogo." Ni kitu gani? Lile kundi la Benyamini linalokuja sasa. "Nitaugeuza mkono wangu juu ya wadogo."

"Mpige Mchungaji." Israeli, kwanza, Israeli walimpiga Mchungaji, wakatawanya kondoo ulimwenguni kote. Lakini Mungu alisema, "Nitageuza mkono Wangu, nipate kuwapata hao wadogo siku ya mwisho." Lini? Wakati upatanisho kwa ajili ya uovu umekwisha fanywa.

56 Israeli wataokolewa, kila mmoja wao. Hebu na tufungue Isaya. Isaya, mlango wa 66 wa Isaya, na usome kwa muda kidogo tu. Na tuone yale Mungu asemayo kuhusu Israeli kuokolewa, kwamba itachukua muda gani kuwaokoa Israeli. Angalia jinsi kutakavyotendeka upesi. Katika Isaya, sura ya 66 na kifungu cha 8. Kama ukitaka kulisoma lote, vema.

*Ni nani aliyesikia neno kama hili? ni nani aliyeona mambo kama haya? Je! nchi yaweza kufanywa na kuzaliwa siku moja—siku moja? Maana Sayuni, mara anapoona utungu, alizaa watoto wake.*

Mara Sayuni alipoona ya kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi wao, alizaliwa mara ya pili, katika siku moja. "Kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi, na kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu, unajisi." Loo, jamani! Walifanya maovu, makosa. Upatanisho ulifanywa kwa ajili ya uovu wao.

57 Namba nne. "Kuleta haki ya milele." Hilo ndilo jambo la nne lililomleta. La nne, yale aliyokuja kufanya, "Ku—kuleta haki ya milele." "Kuishiliza dhambi; upatanisho; na kuleta haki ya milele." Wakati makosa ya Israeli yalipokwisha … Wakati makosa ya Israeli …

Sasa tutaninii… Nataka mshike jambo hili, kwa kuwa tutakapomleta yule mwanamke, na yule joka aliyetupwa, mtarudi moja kwa moja kwenye Andiko lili hili tena. Hakikisheni kuliandika. Wakati makosa ya Israeli yatakapokwisha, Shetani, ambaye ni mshitaki wao na mshitaki wetu, Shetani atafungiwa kuzimu. Wakati nini? Wakati wa kuleta haki ya milele, kitu ambacho hakiwezi kwisha, yote yaliyosababisha kutokuwa na haki yataondolewa.

58 Hebu tufungue Ufunuo mlango wa 20 na kifungu cha 13, kidogo, na tusome hapa kidogo tu. Ufunuo 20, na 13 … La, samahani. Ufunuo … 1 hadi 3, ndivyo ilivyo. Sikuona alama hiyo ndogo katikati yake. Jasho langu hapa linaingia machoni mwangu. Ufunuo mlango wa 20, na hebu tuone. Ufunuo mlango wa 20, na hebu tuone.

*Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, mwenye funguo za kuzimu, na mnyororo mkubwa mkononi mwake.*

... *akamshika yule joka, yule joka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani, akamfunga miaka elfu;*

*Akamtupa katika kuzimu, akamfunga, akatia muhuri juu yake, asipate kudanganya taifa tena, hata ile miaka elfu itimie; na baada ya hayo ... yapasa afunguliwe muda mchache.*

Kufanya ya milele… "Kuleta haki ya milele," Shetani katika kuzimu. Na wakati anapofanya jambo hilo, na kumfungia Ibilisi ambaye amewadanganya watu.

59 Sasa hebu na tufungue nyuma katika Habakuki, mlango wa pili. Habakuki, mlango wa 2. Na sasa tutaona ni kwa nini Yeye alimfunga huyu nyoka wa zamani, na kwa nini yalitendeka, na yale yanayotukia mara tu baada ya kufungwa kwake. Ninapenda jambo hili, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Ina—inatupa ufahamu wa kitu fulani. Habakuki, Habakuki, mlango wa 2 na kifungu cha 14, ninaamini ndivyo ilivyo, ninataka kusoma. Wakati jambo hili litakapotukia… Angalia.

*Kwa maana dunia itajazwa maarifa na utukufu wa BWANA, kama maji yaifunikavyo bahari.*

Loo, jamani! [Ndugu Branham anapiga makofi — Mh.] Whiu! Kwa maneno mengine, wakati adui atakapokuwa ameondolewa, mwisho wa dhambi umekuja, kuletwa kwa haki ya milele kumekuja, Shetani amefungiwa kuzimuni, na maarifa ya Bwana yataijaza dunia kama maji yaifunikavyo bahari. Amina! Utukufu kwa Mungu! Linakuja, ndugu, linakuja! Wanawake watakuwa wanawake wa heshima, na

wanaume watakuwa waungwana. Amina!

Wakati maarifa ya Bwana yatakapoijaza nchi na bahari na mbingu;
Na, lo, moyo wangu unaugua, ukililia siku hiyo ya kufunguliwa kutamu,
Wakati Yesu wetu atakaporudi duniani tena.

Amina! Vema. Sasa, ule Utawala wa Miaka Elfu basi unaendelea. Hapo ndipo ule Utawala wa Miaka Elfu, wakati ule Mji utakapojengwa. Nne … Nina kama Maandiko mengine sita, lakini tutaharakisha. Sasa, tutakaporudi, nitachukua Maandiko haya mengine; lakini kukupa tu wazo la jumla.

60 Namba tano. "Kutia muhuri maono na unabii." Mnaona, huyo Malaika alikuja kutia muhuri maono na unabii.

Ni—ninachukia kusema jambo hili. Lakini, mwandishi mmoja mashuhuri, ambaye nilikuwa nikisoma habari zake hivi majuzi, iwapo hakulivuruga kweli kweli jambo hilo! Yeye alisema ilikuwa ni kitu gani. Sasa, kuonesha tu jinsi ya kijinga …

Loo, samahani. Simaanishi kusema hivyo. Nisamehe. Simaanishi jambo hilo. Kwa kweli sikumaanisha. La.

M—m—mtu asiye na upako, unaona, mtu huyo alisema, "Mnaona hapa ya kwamba maono na unabii daima vilitolewa kwa kanisa la Kiyahudi." Kisha kasema, "Tangu wakati wa Danieli na kuendelea, wakati Danieli alipokuja, ilimaanisha ya kwamba wao hawatakuwa na ono lingine au unabii mwingine." Kasema, "Mambo haya yote siku hizi wanayozungumza juu yake, juu ya kuwa na maono na unabii, yote yalikuwa ni mambo ya Ibilisi, kwamba hakukuwa na kitu kama maono na unabii."

Ndugu, kulikuweko na madazani ya manabii baada ya Danieli. Na kulikuwako na Yohana Mbatizaji. Kulikuwako na Yesu Kristo. Kulikuwako na manabii kupitia Agano Jipya. Kulikuwa na maono. Kulikuwako na Malaika.

Mtu anawezaje kusema hivyo ulimwenguni? Lakini, mnaona, hiyo ni kwa nia ya ubinafsi, kujaribu kuwasukumia watu jambo fulani, kulifanya fundisho dogo la kanisa, ama kitu kidogo kisicho na maana, kuwa kitu kwa watu. Na iwapo watu hawana Roho Mtakatifu, watadanganywa na jambo hilo.

61 Sasa, hebu na tusichukue kile mtu fulani alichosema. Basi, hakuna Maandiko ya kuthibitisha jambo hilo. Hivyo ningewezaje kustahimili jambo hilo? Vema, hebu na tutafute kujua kutia muhuri ni kitu gani hasa. Angalia! Yeye alikuja kufanya jambo hilo, kutia muhuri maono na unabii.

Sasa, hebu na turudi moja kwa moja kwenye Kitabu cha Danieli, mahali tulipokuwa. Katika Kitabu cha Danieli, tunaona vile lilivyosema hasa. Sasa hebu tufungue Danieli sura ya 12. Sasa, tunapofikia Danieli 12, sasa, tunaweza kuanza. Na tunasoma kutoka… Utakapoenda nyumbani, ninataka usome kutoka kifungu cha kwanza na kuendelea. Hebu na tusome tu kutoka kwenye kifungu cha kwanza, hadi cha 4.

*Wakati huo Mikaeli atasimama ... jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako;…*

Sasa, huu ni wakati wa mwisho.

*…na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu…kuwapo taifa…*

Hapo ndipo wakati mpinga-Kristo, huyu mpanda farasi wa Muhuri wa Kwanza, atakapoondoka, wakati jambo hilo linapotukia.

*…hata mpaka wakati huu;.…*

Si katika wakati ule Tito alipoziteka kuta za Yerusalemu. Hiyo ilikuwa tu katika mahali pamoja. Angalia wakati huyu mpinga-Kristo, huyo mtawala aliyekuwa aje, angalia wakati ajapo.

*…na wakati uo huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile.*

Haleluya! "Watu wako," Israeli, "wataandikwa kwenye kitabu."

*Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na madharau ya milele.*

62 Hilo lingalitendeka namna gani kamwe wakati Tito alipoziteka kuta za Yerusalemu? Ingewezaje kuwa ni wakati ule? Haingewezekana. Mnaona, yeye anazungumza juu ya wakati wa mwisho, wakati wa kufufuka. Hiyo ni kweli? Sasa:

*Na walio na hekima watang'aa kama mwangaza wa anga; na hao wawageuzao—waongozao wengi kutenda haki watang'aa kama nyota milele na milele…*

Sikilizeni! Hili hapa, kutiwa muhuri halisi, kwa kweli.

*Lakini wewe, Ee Danieli, yafunge maneno haya, ukakitie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho;*

63 Ni kitu gani? Loo, haleluya! Mnaona jambo hilo, enyi darasa? Huu ufunuo wa Yesu Kristo, na wa Nguvu Zake, wa Kuja Kwake, wa wakati wa mwisho, ulitiwa muhuri mpaka wakati huu. Hilo ndilo alilokuja kufanya. Limefichwa kwa wanachuoni; si ajabu, wanataka kuliweka, "kutiwa muhuri," kule nyuma, kwamba "hakuna manabii," na kila kitu kule nyuma kabisa. Si kweli. Lakini ono, ono hili, limetiwa muhuri mpaka sasa hivi. Na hapo ndipo ninapoweka imani yangu, ya kwamba Mungu atayafunua hayo majuma sabini. Amina! "Kitie muhuri," Yeye alisema, "mpaka wakati wa mwisho. Yafunge Maneno na ukifunge Kitabu mpaka wakati wa mwisho."

64 Alifanya nini? Kutia muhuri maono na unabii! Danieli alikuwa ametabiri mambo haya. Alikuwa ameyaona katika ono, ndipo Malaika akashuka akaja kutia muhuri hilo ono, na kutia muhuri unabii. Wao wanaweza kuusoma, lakini hawawezi kuufahamu, mpaka wakati wa mwisho. Wakati wa mwisho, wakati wa mwisho ni nini? Ule mwisho wa lile juma la sabini, wakati yule mtawala, mpinga-Kristo, atakapofunuliwa, kwenye wakati huu, akijifanya mwenyewe Mungu. Tunajuaje ya kwamba jambo hili limetiwa muhuri kwa wakati huu? Danieli ndiyo kwanza amalize; hii ni sura ya mwisho ya Danieli.

65 Dada Simpson aliniambia alasiri ya leo, akasema, "Ndugu Branham, nilisoma Kitabu chote cha Danieli. Si—sikujua kamwe mengi zaidi wakati nilipokoma, nilipokimaliza, kuliko niliyojua wakati nilipoanza." Hii hapa, Dada Simpson, kama uko hapa usiku wa leo. Ninaamini ninamwona ameketi pale. Sikusema kitu kwenye lile trela. Nilinyamaza, maana nilifikiri labda nitalifikia.

Lakini, lile ono ambalo Danieli aliliona, kule chini kando ya mto, lilitiwa muhuri, "mpaka wakati wa mwisho." Ni … Hebu niendelee tu na kulisoma hapa. Mnaona?

*Lakini wewe, Ee Danieli, yafunge maneno haya, ukakitie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho; wengi wataenda mbio huko na huko, na maarifa yataongezeka.*

*Ndipo mimi, Danieli, nikatazama, na kumbe, wamesimama wengine . . . wawili, . . . mmoja ukingoni mmoja … mwa mto upande huu, na mmoja ukingoni mwa mto upande wa pili.*

*Na mmoja akamwuliza yule mtu aliyevikwa nguo za—za kitani, aliyekuwa juu ya maji ya mto, Je! itakuwa muda wa miaka mingapi hata mwisho wa mambo haya ya ajabu?*

Sasa sikilizeni.

*Nami nikamsikia yule mtu aliyevikwa nguo za kitani, aliyekuwa juu ya maji ya mto, hapo alipoinua mkono wake wa kuume na mkono wake wa kushoto kuelekea mbinguni; akaapa kwa yeye aliye hai milele na milele, ya kwamba itakuwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati;…*

Sasa, tupate vizuri—vizuri kabisa, "Wakati, nyakati mbili, na nusu wakati." *Sasa angalia tutakapofikia kwenye majuma sabini ya Danieli, jinsi jambo hilo litakavyotokea. Hapo ndipo ile siri itakapofunuliwa.* Vema. "Wakati, nyakati mbili, na nusu wakati."

*…tena yeye atakapokuwa…*("yeye" kijina cha mtu sasa, mpinga-Kristo)… *amekwi-… amekwisha kuvunja—kuvunja nguvu za hao watu watakatifu*, (hapo ni wakati atakapolivunja agano katikati ya juma), *ndipo mambo hayo yote yatakapotimilizwa.* (Amina.)

*Nami nikasikia, lakini sikuelewa; ndipo nikasema, E…Bwana wangu, mwisho wa mambo haya utakuwaje?*

*Akasema, Enenda zako, Danieli; maana maneno haya yamefungwa, na kutiwa muhuri, mpaka wakati wa…*

[Ndugu Branham anatulia. Kusanyiko linasema, "Mwisho!" — Mh.] Loo, msisahau jambo hilo!

… Mpaka wakati wa mwisho.

*Wengi watajitakasa, na kujifanya weupe, na kusafika; bali wabaya watatenda mabaya; wala hataelewa mtu mbaya awaye yote; bali wao walio na hekima ndio watakaoelewa.*

66 Ujumbe wa wakati wa mwisho utafunua jambo hilo; wakati wa mwisho wa kanisa. Utukufu! Whiu! Haya basi! Loo, jamani! Linanitikisa, kuwazia jambo hilo, ile siri! Mambo ambayo kanisa la ulimwengu huyapuuza, na kusema, "Ni upuuzi." Ile siri ya Yesu Kristo alikuwa ni nani; si Nafsi ya tatu, si Nafsi ya pili, si Nafsi ya tatu, lakini ni ile Nafsi ya Mungu. Siri hizi nyingine zote za Mungu zitafunuliwa, kwa sababu zimeandikwa hapa katika kitabu Hiki, na kufunuliwa kwa kizazi cha wakati wa mwisho. Hawawezi kuziona

zaidi katika maseminari, na mashule, na madhehebu, kuliko vile Wayahudi wangeweza kumwona Yesu kwamba ni Masihi. Si ajabu wao wanajaribu kufikiri ya kwamba wewe ni mwenda wazimu. Si ajabu wanafikiria wewe ni mpumbavu. Si ajabu hawawezi kufahamu kwa nini hulii pamoja nao kama kuku. Kwa sababu, kuna Nguvu na ono nyuma ya jambo hilo, Neno la Mungu lililofunuliwa, kuliweka Kanisa katika utaratibu kwa ajili ya Kunyakuliwa na kwenda Nyumbani. Ndiyo. "Wengi wataenda mbio huko na huko, na maarifa yataongezeka." Hakika.

67 Sasa, ni jambo gani lingine ambalo lingejulikana? Angalia siku hizi, kwenye makanisa. Hili hapa. Natumaini halitaumiza, bali sina budi kulisema. Kufanya …

Katika siku hiyo, mpinga-Kristo atainuka.

Sasa, kumbukeni, tutakapofikia kwenye ile Muhuri, ya kwamba mpinga-Kristo anapanda farasi juu ya Mihuri hiyo. Danieli alinena habari zake hapa, "Mfalme atakayekuja." Yeye angekatiliwa mbali, Yesu angekataliwa, kufanya upatanisho kwa ajili ya watu. Lakini, "Mfalme yule ambaye angesimama, ambaye angesababisha chukizo la uharibifu," huyo alikuwa ni Rumi, kupitia kwa Tito. Na wakati huu, ni mfalme anayetoka Rumi, atakayefanya jambo hilo. Naye atafunuliwa katika siku ya mwisho, sasa sikilizeni, "akijifanya mwenyewe ni Mungu," kama vile Roho Mtakatifu anavyotuonya katika Wathesalonike wa Pili, ya 2

Hebu tuiendee tu, Wathesalonike wa Pili, ndipo hamtachukua neno langu ila Neno la Mungu. Wathesalonike wa Pili, mlango wa 2 na kifungu cha 12. Hebu tuone. Wathesalonike wa Pili, mlango wa 2 na kifungu cha 12. Hebu tuone. Hebu na tuanzie juu ya hilo, kifungu cha 7.

> *Maana ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi;…*

(Huyu ni Paulo akinena, kwa Roho Mtakatifu.)

> *… lakini—lakini yuko yeye azuiaye sasa, hata atakapoondolewa.*

"Yeye" hapa ni nani? Kuna mtu anayejua? Roho Mtakatifu, "Yeye azuiaye."

> *Hapo ndipo* (wakati) *atakapofunuliwa yule asi,…*

Lini? Wakati ule Roho Mtakatifu anapoondolewa tu, ambaye yuko tayari kuondoka sasa hivi. Yeye anaondoka kwa ajili gani? Akiondoka pamoja na Kanisa. "Atakapofunuliwa!" Paulo akinena, chini ya uvuvio.

> *…ambaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake, na kumwangamiza kwa ufunuo wa kuwapo kwake;* (yule mwovu, bila shaka)

> *Yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo;*

"Sisi ndio kanisa lililo kuu sana kuliko yote. Tuna hili. Tuna hili. Ninyi nyote unganeni pamoja, mnaona. Sisi ndio tulio wakuu sana kuliko wote." Maajabu ya uongo!

> *Na katika ... madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa.*

> *Kwa hiyo Mungu amewaletea nguvu za upotevu, wauamini uongo—wauamini uongo;*

> *Ili wahukumiwe…ambao hawakuiamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu.*

Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Loo, jamani! Sasa, Paulo akinena. Wakati ambapo Muhuri wa Mungu unapofunuliwa, Roho Wake, Jina Lake, neema Yake, siri hizi nyingine zote kuu zinazofunuliwa sasa, mipango ya Kunyakuliwa kwa Kanisa Lake; kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kumefanya jambo hili. Hayo ndiyo ambayo Yeye amefanya katika siku za mwisho.

68 Sasa, hebu tuone. Je! Tuna wakati wa hili la mwisho? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] La sita, "Kumtia mafuta Yeye aliye Mtakatifu sana." Loo, jamani! Hili hapa moja! Jambo la mwisho atakalofanya, ni lipi? Sasa, hebu na turudi nyuma katika Danieli, tuone yote atakayofanya papa hapa. "Majuma sabini." Ni kitu gani kitakachotimizwa katika wakati huu? Vema.

> *…umeamriwa juu ya watu wako, na…ya mji wako mtakatifu, ili kukomesha makosa*, (makosa ya watu hao),… *na kuishiliza dhambi*, (za watu hao), *na kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu wao, na kuleta haki ya milele,* (kwa ajili ya Wayahudi), *na kutia muhuri maono na unabii*, (mpaka wakati wa mwisho), *na kumtia mafuta yeye aliye Mtakatifu sana.*

Hizo ndizo sababu sita za kuja Kwake.

69 Sasa, "kumtia mafuta aliye Mtakatifu sana." Sasa, hili linaweza kuwa kwa muda mdogo tu, kwa wengi wenu ninyi waalimu, lakini sasa tulieni tu kwa muda kidogo, mwone jinsi litakavyotokea.

Huku ni kutiwa mafuta, si kwa mwanadamu. Yesu tayari ametiwa mafuta. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Kitabu cha Matendo kilisema Mungu alimtia Yesu mafuta kwa Roho Mtakatifu; alienda kila mahali akitenda mema, akiwaponya wagonjwa na kadhalika. Yesu yuko, tayari. Yeye ni Masihi. Na *Masihi* maana yake ni "Mtiwa mafuta." Hiyo ni kweli? Lakini hapa katika wakati wa mwisho, Yeye atamtia mafuta aliye Mtakatifu sana.

"Yeye aliye Mtakatifu sana" ni kitu gani?" Nionavyo mimi, na ninaamini ninaweza kulithibitisha kwa Maandiko, ni kumtia mafuta "yeye aliye Mtakatifu sana," ambapo itakuwa ni Maskani itakayotumiwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Sasa sikilizeni, mwone kwa nini nimelipata. Kama ilivyoelezewa katika Ezekieli, sura ya 4, ile … La, ninamaanisha sura ya 43, aya ya 1 na ya 6. Hebu na turudi kwenye Ezekieli tuone jinsi anavyoelezea ule Utawala wa Miaka Elfu, jinsi watakavyotia mafuta ninii… Ezekieli 43, na hebu tusome kidogo hapa sasa na tuone yale atakayofanya katika huu Utawala wa Miaka Elfu, kutia mafuta. Katika Ezekieli 43, vema, na sasa hebu tuanzie kifungu cha 1, hadi cha 6. Mnaweza kuisoma yote mfikapo nyumbani, bila shaka, ninyi ambao mnayaandika, Ezekieli 43. "Baadaye …"

70 Sasa, angalia, wasifu wa lile Hekalu litakalojengwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Sasa, mtu ye yote, msomaji ye yote anayejua, ya kwamba Ezekieli sura ya 40, mpaka kufikia kama ya 44, si kitu duniani ila ni Hekalu la ule Utawala wa Miaka Elfu likijengwa duniani, (mtu ye yote anafahamu jambo hilo, mnaona), wakati utukufu wa Mungu utalijaza, na kadhalika namna hiyo. Sasa tunaninii…tutatoa tu wasifu wa hilo Hekalu katika mlango wa 43, na kifungu cha 1 hadi cha 6.

> *Kisha akanileta mpaka langoni, yaani, lango lile linaloelekea upande wa mashariki;*
>
> *Na tazama, huo utukufu wa ... Mungu wa Israeli ulitokea kwa njia ya mashariki; na sauti yake ilikuwa kama mshindo wa maji mengi, nayo nchi iling'aa kwa utukufu wake.*
>
> *Na maono niliyoyaona yalikuwa kama maono niliyoyaona, ni kama maono niliyoyaona nilipokuja kuuharibu mji; nalo ono nililoona lilikuwa kama ono nililoona karibu na mto wa Kebari; nikaanguka kifudifudi.*
>
> *Na huo utukufu wa BWANA—utukufu wa BWANA ukaingia ndani ya nyumba, kwa njia ya lango lile lielekealo upande wa mashariki.*
>
> *Kisha Roho ikaniinua, ikanichukua mpaka ua wa ndani; na tazama, utukufu wa BWANA uliijaza nyumba.*
>
> *Nikasikia sauti ya mmoja asemaye nami, itokayo katika nyumba hiyo; na mtu huyo akasimama karibu nami.*

71 Kutia mafuta, kutia mafuta lile Hekalu kwa ajili ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Sasa angalia katika Mambo ya Walawi. Sasa angalia jinsi lilivyowekwa wakfu katika Mambo ya Walawi. Sasa, kama tukirudi katika Mambo ya Walawi, tunaona ya kwamba Musa alilitia mafuta lile hekalu. Hebu turudi nyuma wakati tungalipo kwenye jambo hili. Tuna muda kiasi hicho. Hebu na turejee katika Mambo ya Walawi tuone wakati ule Musa alipolitia mafuta lile hakalu, katika Mambo ya Walawi mlango wa 8.

Loo, ninapenda tu kulinganisha Maandiko haya kwa Maandiko. Je! mnalipenda? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Ndipo u—utapata ninii—ninii—fununu juu ya yale—yale tunayotafuta na yale tunayofanya. Basi, kila mmoja wenu anatambua ya kwamba tunatumia tu Maandiko mara kwa mara, katika jambo hilo.

72 Sikiliza, sura ya 8 ya Mambo ya Walawi, nami nimeyaandika chini hapa, mlango wa 10. Angalia Mambo ya Walawi 8:10. Hebu tuone.

> *Kisha Musa akatwaa hayo mafuta mtakatifu ya kutia, kisha akamimina mafuta ya kutia, akatia mafuta maskani, na vyote vilivyokuwamo, na kuvitakasa.*
>
> *Kisha ... akanyunyizia hayo mafuta juu ya madhabahu mara saba, … kuitia mafuta madhabahu na vyombo vyake vyote, na birika na tako lake, ili ... kuvitakasa.*
>
> *Kisha akamimina mafuta…ya kutia kichwani mwake Haruni, na kumtia mafuta, ili amtakase.*

Musa, jangwani, akitakasa, ama akitia mafuta ile maskani ya kuabudia, kwa ajili ya wana wa Israeli walipokuwa katika safari yao. Ilitiwa mafuta.

73 Sasa, katika Mambo ya Nyakati ya Pili, tufungue, nasi tutaona kule kuwekwa wakfu ambapo wakati Roho Mtakatifu alipokaa kwenye hiyo maskani, na tuone jambo lililotukia sasa. Katika Mambo ya Nyakati

Pili mlango wa 5, na hebu tuanzie kwenye kifungu cha 13. Mambo ya Nyakati ya Pili sura ya 5, tuanzie aya ya 13.

> *Basi ... ikawa, wenye panda na waimbaji walipokuwa kama mmoja ... wakisikizisha sauti moja ... ya kumsifu na kushukuru BWANA; nao wakipaza sauti zao pamoja na panda na matoazi na vinanda, wanamsifu BWANA, wakisema, Kwa kuwa ni mwema; kwa maana fadhili zake ni za milele; ndipo nyumba ikajawa na wingu, naam, nyumba ya BWANA;*

> *Hata makuhani walisimama…makuhani hawakuweza kusimama ili kufanya huduma yao, kwa sababu ya lile wingu; kwa kuwa nyumba ya Mungu imejaa utukufu wa BWANA.*

Mungu aliingia madhabahuni ambapo panatakiwa kutiwa mafuta, na ilitolewa Kwake kusudi watu waje waabudu. Kwa hiyo, kutia mafuta, si "mahali pako patakatifu," lakini "kutia mafuta mahali Patakatifu sana." Na tunaona, ya kwamba, Yerusalemu Mpya ndio "mahali Patakatifu sana." Na kutiwa mafuta kutakuwa juu ya Yerusalemu Mpya ukishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arui aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Kutiwa mafuta kutakuwa juu yao.

74 Sasa, wakati Zerubabeli alipoliweka wakfu hekalu lake, baada ya kujengwa upya, halikutiwa mafuta tena, kwa sababu lilikuwa tayari limetiwa mafuta; na lilikuwa limebomolewa, nalo lilikuwa ndiyo kwanza tu lijengwe upya tena. Lilikuwa limepatwa na uharibifu. Lilikuwa limejengwa upya tena na kusimamishwa, kwa hiyo hapakuwepo na kutiwa mafuta kwake tena. Lilipotiwa mafuta wakati mmoja, huko kulitosha sikuzote, nako kunaendelea mpaka wakati uu huu. Lakini wakati Mungu atakapoisimamisha Maskani ya ule Utawala wa Miaka Elfu, Yeye atapatia mafuta mahali Patakatifu sana; si mahali "pako patakatifu," lakini "Patakatifu sana."

75 Lakini wakati Mfalme atakapochukua Kiti Chake cha enzi kwa ajili ya ile miaka elfu moja, (utukufu!) limekwisha sasa. Kutiwa mafuta kwa kwa mahali Patakatifu sana litakuwa ndilo jambo la mwisho litakalotukia. Wakati ile Maskani itakaposimamishwa; ufufuo umekuja; Wayahudi wamerudi; Kristo na Bibi-arusi Wake amekuja; Wayahudi, wale mia na arobaini na nne elfu wametiwa muhuri; ule Utawala wa Miaka Elfu umetokea. Kutakuwako na kutiwa mafuta wakati mahali Patakatifu sana patakapotiwa mafuta; patakatifu, Patakatifu pa patakatifu, na Patakatifu sana. Wakati, mahali Patakatifu sana ni pale kwenye madhabahu ambapo Mungu aliishi, katikati ya wale Makerubi. Na, wakati huu, Kristo ataketi kwenye mahali Patakatifu sana, akiwa ametiwa mafuta. Wala hawatahitaji jua pale, kwa maana Mwana-Kondoo katikati ya ule Mji atakuwa ndiye Nuru. Jua halitatua kamwe kwenye Mji huo, kama vile mzee Mjomba Jim alivyokuwa akisema mara kwa mara. Wala halitatua, kwa maana Kristo ndiye atakayekuwa hiyo Nuru, Mtiwa Mafuta. Naye Mfalme atakuja na kukitwaa Kiti Chake cha Enzi kwa muda wa miaka elfu moja, kutawala.

76 Yeremia 3:12-18, zote pamoja, hebu na tuisome. Huko katika Yeremia sura ya 18, ninaamini. Naam. La, sura ya 12, samahani, sura ya 12 ya Yeremia, na hebu tuanzie kwenye—kwenye…Yeremia 3, samahani. Yeremia 3, nimekwisha kuandika hapa chini, ambapo, nilipokuwa nikisoma, Roho Mtakatifu akiniongoza mimi kutoka mahali pamoja kwenda pengine, nilijitahidi kuandika tu vizuri nilivyoweza. Yeremia 3, halafu 12 hadi 18, pamoja. Hebu na tulisome.

> *Enenda, ukatangaze maneno haya kuelekea upande wa kaskazini, ukaseme, Rudi, Ee Israeli mwenye kuasi, asema BWANA, sitakutazama kwa yangu—yangu … sitakutazama kwa hasira; maana mimi ni mwenye rehema, asema BWANA, sitashika hasira hata milele.*

> *Ungama uovu wako tu; ambao umemwasi BWANA, Mungu wako, na njia zako zimekuwa nyingi kuwaendea wageni chini ya kila mti wenye majani mabichi, ...*

Hivyo ndivyo walivyofanya, kutoka mashariki, magharibi, kila taifa. Mnaona?

> *…wala hamkutii ile sauti, sauti yangu, asema BWANA.*

"Rudini!" Sikilizeni jambo hili.

> *Rudini, enyi watoto wenye kuasi, asema BWANA; maana mimi ni (m-mu-m-e)…mume wenu; …*

"Macho yao yalipofushwa, kwa maana niliwapa Mataifa nafasi. Lakini, rudini, kwa maana mimi ni mume wenu."

> *… nami nitatwaa mtu mmoja wa mji mmoja, na wawili wa jamaa moja, …*

Si wote wanaojiita Wayahudi wataingia. Lakini hilo kundi lililoteuliwa litaingia, yule Benyamini mdogo aliyeshuka kule chini mbele ya Yusufu, kundi lile kutoka katika kila taifa, mtu mmoja kutoka katika mji mmoja, na kutoka katika jamaa moja.

> *…nami nitawaleta hata Sayuni;*

*Nami nitawapa ninyi mchungaji wanipendezao moyo wangu, watakaowalisha kwa maarifa na fahamu.*

*Kisha itakuwa, mtakapoongezeka na kuwa wengi katika nchi hiyo, katika siku hizo, asema BWANA, siku zile hawatasema tena, Sa—sanduku la agano la BWANA; wala halitaingia moyoni; wala hawatalikumbuka, wala ha—hawatalizuru, wala hayatafanyika hayo tena.*

*Wakati ule watauita Yerusalemu kiti cha enzi cha BWANA;* (kwa kuwa atakuwako kule, mnaona), *na taifa lote watakusanyika* (haleluya) *huko Yerusalemu, kwa ajili ya jina la BWANA, kwenda Yerusalemu: wala hatakwenda tena kwa ukaidi wa moyo wao mbaya.*

77 Hapo ndipo Mji huo utakapotiwa mafuta. Hapo ndipo Yerusalemu Mpya itakapotiwa mafuta. Na mataifa yote ya Mji … Katika Ufunuo sura ya 22, inasema malango hayatafungwa usiku, maana hakutakuweko na usiku kule. Na wafalme wote wa dunia wataleta heshima na utukufu wao katika Mji huu. Kuta zake zitakuwa za mawe ya yaspi na akiki, namna kumi na mbili za mawe; na malango kumi na mbili yatakuwa ya lulu tupu, kila lango. Hakutakuweko na haja ya mshumaa humo. Hakutakuweko na haja ya nuru ya jua tena, kwa maana Mwana-Kondoo aliye katikati ya ule Mji atakuwa ndiye Nuru Yake. Naye atawaongoza watu Wake kwenye Uzima wa milele. Kutakuweko na miti miwili itakayokuwa imesimama, mmoja kwa kila upande wa mto, nayo itakuwa kwa ajili ya kuponywa kwa taifa. Huyo ni Ule uliopakwa mafuta utakaokuja, ule Mji Mtakatifu ukishuka kutoka kwa Mungu kutoka Mbinguni, ukija duniani.

78 Hebu na tuchukue sasa jambo litakalotendeka wakati huo. Loo, mnalipenda? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hebu na tufungue Isaya 65, kwa dakika moja. Ni zuri sana hatuwezi kuliruka. Ni zuri sana hatuwezi kuliacha. Huenda ikawa ni joto kidogo, lakini hebu tuendelee tu.

Isaya 65, sikilizeni jambo litakalotukia katika wakati huo. Na hebu ujiulize tu mwenyewe, ewe rafiki mwenye dhambi, kama wewe—kama ungeweza kukosa jambo hili. Isaya 65, hebu tuanzie kwenye kifungu cha 17 hivi. Sikilizeni, kila mtu, kwa makini sasa. Hii ni katika wakati wa ule Utawala wa Miaka Elfu, wakati mahali palipo Patakatifu sana patakapotiwa mafuta.

*Maana, tazama, mimi naumba mbingu mpya na ... nchi mpya, na mambo ya kwanza hayatakumbukwa, wala hayataingia moyoni.*

*Lakini furahini, mkashangilie…hata kwa ajili ya hivi niviumbavyo; maana, tazama, naumba Yerusalemu… naumba Yerusalemu* (hiyo ni kusema Yerusalemu Mpya) *uwe shangwe, na watu wake wawe furaha.*

Kule kutia mafuta ni nini? Furaha ya Bwana.

*… naumba Yerusalemu uwe shangwe, na watu wake wawe furaha. Nami nitaufurahia Yerusalemu, …*

Mfalme kwenye kile Kiti cha Enzi, katika ule utukufu wa kile Kiti cha Enzi, Kiti cha Enzi cha Milele, na watu wa Milele pamoja na furaha ya Milele katika Mji wa Milele! Loo, jamani!

*Nami nitaufurahia Yerusalemu, nitawaonea shangwe watu wangu; na sauti ya kulia haitasikiwa ndani yake tena, wala sauti ya kuomboleza.*

*Hatakuwepo tena mtoto wa siku chache, wala mzee asiyetimia siku zake; kwa maana mtoto atakufa mwenye umri wa miaka mia; bali mtenda dhambi mwenye umri wa miaka mia atalaaniwa.*

*Nao watajenga nyumba, na kukaa ndani yake; ... watapanda mizabibu, na kula matunda yake.*

*Hawatajenga, akakaa mtu mwingine ndani yake;* (hiyo ni kusema unakufa na mwanao anapachukua mahali pako)…*jenga, akakaa mtu mwingine ndani yake; hawatapanda, akala mtu mwingine; maana kama siku za mti ndivyo zitakavyokuwa siku za watu wangu, na wateule wangu wataifurahia kazi ya mikono yao muda wa siku nyingi.*

*Hawatajitaabisha kwa kazi bure, wala hawatazaa kwa taabu; kwa sababu wao ni wazao wa hao waliobarikiwa na BWANA, na watoto wao pamoja nao.*

*Na itakuwa ya kwamba, kabla hawajaomba, nitajibu;…* (Huo upako wenye utukufu, huko nyuma ya Makerubi!) *na wakiwa katika kunena, nitasikia.*

*Mbwa mwitu na mwana-kondoo watalisha pamoja,…simba atakula majani kama ng'ombe; na mavumbi yatakuwa chakula cha nyoka. Hawatadhuru wala kuharibu katika mlima wangu mtakatifu wote, asema BWANA.* (Je! unaweza kukosa jambo hilo? La!)

79 Ruka moja nyuma kwa moja hapa tena, na Isaya akinena tena, kwenye mlango wa 11, kifungu cha 1

hadi ya 9. Sikilizeni yale anayosema hapa tena, wakati anapolipata lile ono, baada ya yeye kuwaona hao wanawake, jinsi watakavyokuwa wanatenda katika siku za mwisho. Ni- … Vema, Isaya 11, hadi 1.

> *Basi litatoka chipukizi katika shina la Yese,… Tawi litakalotoka katika mizizi yake* (Huyo alikuwa ni nani? Kristo.)…*katika mizizi yake:*
>
> *Na roho ya BWANA atakaa juu yake, roho ya hekima na ufahamu, roho ya shauri … uweza, roho ya maarifa na … kumcha BWANA;*
>
> *Na furaha yake itakuwa katika kumcha BWANA; wala hatahukumu kwa kuyafuata ayaonayo kwa macho yake, wala…kwa kuyafuata ayasikiayo kwa masikio yake;*
>
> *Bali kwa haki atawahukumu maskini, naye atawaonya uovu wao wanyenyekevu wa dunia kwa adili; naye ataipiga dunia kwa fimbo ya kinywa chake, na kwa pumzi ya midomo yake atawaua wabaya.*
>
> *Wenye haki watakuwa mshipi wa viuno, na waaminifu mshipi wa kujifungia.*
>
> *Na mbwa-mwitu atakaa pamoja na mwana-kondoo, na chui atalala pamoja na mwana-mbuzi* (huyo ni mbuzi); *ndama na mwana-simba na kinono…ama ndama, ama simba na kinono watakuwa pamoja, na mtoto mdogo atawaongoza.*
>
> ... *Ng'ombe na dubu watalisha pamoja; ... watoto wao watalala pamoja; na simba atakula majani kama ng'ombe.*
>
> *Na mtoto anyonyaye atacheza penye tundu la nyoka, na mtoto aliyeachishwa atatia mkono wake katika pango la fira.*
>
> *Hawatadhuru ama hawataharibu katika milima yangu yote mitakatifu; maana dunia itajawa na kumjua BWANA, ... kama vile maji yafunikavyo bahari.*

A-ha! Hiyo ni katika ule Yerusalemu Mpya. Hiyo "mpya." Tawi, hapa, linahusu, tawi la Daudi. "Yeye ni Tawi na Mzao pia."

80 Sasa, baada ya jambo hili, Bibi-arusi anatokea. Baada ya yale majuma sabini, Bibi-arusi anaonekana katika ufunuo mlango wa 19, kifungu cha 1 na cha 16. Yeye anawasili pamoja na Bwana-arusi Wake, yule Mfalme mwenye nguvu. Loo, jamani! Sijui kama tutalipata lote ama hatutalipata. Tumeinanii tu…

Vema, hebu tusome tu sehemu ya hili, hata hivyo. Hapa ndipo Bibi-arusi atakapokuja, baada ya jambo hili. Mnaona? Baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu kuanza, ndipo Kristo anarudi pamoja na Bibi-arusi Wake. Vema, 1 hadi 16, na mlango wa 19.

> *Na baada ya mambo haya …*

Baada ya Dhiki hii; baada ya zile Ole; baada ya ile Mihuri; baada ya yale Mapigo; baada ya kutupwa kwa Shetani; baada ya kuanzishwa kwa ule Utawala wa Miaka Elfu. Angalia!

> *... baada ya mambo hayo nikasikia sa…sauti kama sauti ya makutano mengi, mbinguni, ikisema, Haleluya; Wokovu na utukufu…heshima…nguvu zina Bwana Mungu wetu;*
>
> *Kwa kuwa hukumu yako ni za kweli na za haki; maana alimhukumu yule kahaba mkuu aliyeiharibu nchi kwa uasherati wake, na kuipatiliza damu ya watumwa wake mkononi mwake.*
>
> *Wakasema mara ya pili yeye…wao…Na wakasema mara ya pili, Haleluya. Na moshi wake hupaa juu hata milele na milele.*

Hilo ni lile kanisa kahaba la kale, "moshi wake ulipaa juu."

> *Na wale wazee ishirini na wanne, na wale wenye uhai wanne, wakasujudu na kumwabudu Mungu, aketiye katika kile kiti cha enzi, wakisema, Amina.* Haleluya.
>
> *Sauti ikatoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Msifuni Mungu wetu—Msifuni Mungu wetu, enyi watumwa wake wote, na ninyi mnaomcha, wadogo kwa wakuu.*
>
> *Nikasikia sauti kama sauti ya makutano mengi,…*

Sikilizeni! Angalieni hapa, Kanisa. Baada ya kupaa juu kwenye sura ya 3, Huyu hapa anakuja. Mnaona? Na sasa aya ya 6.

> *Nikasikia sauti kama sauti ya makutano mengi, na kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi yenye nguvu, ikisema, Haleluya; kwa kuwa Bwana Mungu wetu, Mwenyezi,*

*amemiliki.*

Haleluya! Angalia! Arusi ya Mwana-Kondoo inakuja sasa. Huyu hapa anakuja.

*Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari.* (Huyu hapa anakuja, Bibi-arusi na Bwana Arusi pia.)

*Naye amepewa kuvikwa kitani nzuri, ing'arayo, safi; kwa maana kitani nzuri hiyo ni matendo ya haki ya watakatifu.*

*Naye akaniambia, Andika, Heri walioalikwa karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo. Akaniambia, Maneno haya ni maneno ya kweli ya Mungu.*

*Nami nikaanguka chini mbele ya miguu yake, ili nimsujudie; akaniambia, Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako,…ndugu zako walio na…ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Msujudie Mungu. Kwa maana ushuhuda* (wa Kristo) *wa Yesu ndio roho ya unabii.*

*Kisha nikaziona mbingu zimefunuka, na…farasi mweupe,…* (loo, jamani!) *yeye mwenye kumpanda, aitwaye Mwaminifu na Wa-kweli, naye…haki ahukumu na kufanya vita.*

*Na macho yake yalikuwa kama mwali wa moto, na juu ya kichwa chake vilemba vingi;…*

Yeye alivikwa taji kama nani? "Mfalme wa Wafalme."

*…naye alikuwa ana jina lililoandikwa, asilolijua mtu ila ... yeye mwenyewe.*

*Naye amevikwa vazi lililochovywa katika damu, na jina lake aitwa, Neno la Mungu.*

"Hapo mwanzo alikuwepo Neno, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu." Alikuwa ni nani? Yesu.

*…na jina lake aitwa, Neno la Mungu.*

*Na majeshi yaliyo mbinguni wakamfuata, wamepanda farasi weupe na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe, safi.* (Utukufu! Huyu hapa Bibi-arusi anakuja) *Na upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige taifa kwa huo. Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi.*

*Naye alikuwa ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA MFALME, NA BWANA WA BWANA.*

81 Ilikuwa ni kitu gani? *Watu Wake walikuwa ndiyo kwanza wamvike taji Mfalme wa mfalme, na Bwana wa mabwana. Akirudi kwenye Hekalu Lake takatifu, ametiwa mafuta na Uwepo wa Mungu, kuishi na kutawala katika ule Utawala wa Miaka Elfu pamoja na Kanisa Lake.* Amina! *Kule kuonekana, pamoja na Mfalme mwenye nguvu, kuchukua mahali Pake kando Yake, lile Hekalu jipya la mfalme lililotiwa mafuta.*

Sasa zile sababu sita za kusudi la Ufunuo 6:1 mpaka Ufunuo 19:21 zimetimizwa.

82 Sikilizeni sasa, katika kufunga. Ile Mihuri Saba, Baragumu Saba, Vitasa Saba, Ole Tatu, mwanamke katika jua, kutupwa kwa Ibilisi, ama lile joka jekundu, vinatokea katikati ya nyakati hizi katika wakati wa ile Dhiki kuu. Msisahau jambo hilo. Mambo haya yote yanatukia wakati huu.

Lakini hizi hapa zile sababu sita za kusudi la Kuja Kwake. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Ni wakati mzuri namna gani unaowangoja hao wampendao Bwana! Ninakwambia, ewe rafiki, hatuwezi kukubali kukosa jambo hilo. Usikose jambo hilo, kwa cho chote ufanyacho. Kuwa na hakika!

83 Sasa, Jumapili ijayo, Bwana akipenda, ninataka kuwasilisha, Bwana akinisaidia, kuonyesha ni mahali gani hasa kila moja ya hizo siku saba, mahali zilipotimia, kuleta jambo lili hili—jambo lile lile nililoleta leo, na kuweka nyakati hizo saba, majuma saba, majuma sabini moja kwa moja kwenye mahali pa ile madhabahu ya Kiyahudi, na kuonyesha ni mahali gani hasa tunapoishi hapa mwishoni, Bwana akipenda.

84 Je! Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Ungeweza kustahimili kukosa Mbinguni? ["La."] Tuko katika wakati wa mwisho!

Yeye anakuja kufanya nini? Jambo la kwanza litakalotukia, kabla Yesu hajaja duniani, jambo la kwanza litakuwa ni nini? Kanisa litafanywa (nini?) litanyakuliwa! Je! Yesu atakuja duniani na kutembea makaburini, na kupeana mikono na baba na mama, azungumze nasi sote hapa, kisha apae juu? La!

Itakuwaje? Ninii … Tunawaambia jambo hili, kwa—kwa Neno la Bwana, "Ya kwamba sisi tulio hai, tuliosalia…" Wathesalonike wa Pili, mlango wa 5, "Sisi tulio hai, tuliosalia hata kuja kwa Bwana, hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa maana parapanda ya Mungu italia; waliokufa katika

Kristo watafufuliwa kwanza: kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani." Tutanyakuliwa katika dakika moja, katika kufumba na kufumbua jicho. Kwenye wakati huo, hilo linamalizia Wakati wa Kanisa.

85 Ndipo, chini hapa duniani Mungu anaanza kuwashughulikia Wayahudi. Kutakuwako na manabii wawili. Mlango wa 11, tutalichukua hilo. Manabii wawili waliotiwa mafuta, kama Eliya na Musa, ambao ninafikiri ndio. Nao wataleta mapigo makubwa, baada ya kuona ya kwamba wao wameungana, na Rumi imevunja lile agano, yule mtawala.

Katikati ya juma hili la sabini, itavunja agano lake na Rumi, ama Rumi itavunja agano lake na Israeli, na jambo hilo litasababisha chukizo kuanza kutawanyika. Na kutakuweko na gharika kuu, wakati wale masalia ya Wamataifa, wanawali waliolala… Yule joka, Rumi, alitoa maji katika kinywa chake, kufanya vita na masalia ya uzao wa mwanamke waliotii amri za Mungu. Rumi itafanya jambo hilo.

86 Muungano wa makanisa utawakusanya pamoja, na kuwaleta Wayahudi katika muungano huu, na kuwarudisha kwenye ibada za hekalu lao tena, katika BWANA ASEMA HIVI kutoka kwenye Biblia, nao watakuwa na kanisa lao wenyewe. [Ndugu Branham anapiga mimbara mara kadha—Mh.]

Wao ni nini sasa? Nimelipata sasa hivi. Ni jipya. Wao sasa ni taifa, linalotambuliwa. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Lakini hawana bado ibada zao za hekaluni. Na hapo watakapoanzisha ibada za hekaluni, Kanisa litakuwa limeondoka. Mungu atakuwa akiwashughulikia Wayahudi kama taifa. Halafu wakati watakapoletwa katika muungano huu, Rumi italivunja katikati ya mwaka wa sabini, miaka mitatu na nusu, yeye atavunja agano hilo nao, na kusababisha chukizo la uharibifu kusambaa hata mwisho. Ndipo atawachukua Waprotestanti pamoja na Wayahudi, na kuwatesa. Katika wakati huo, manabii hawa wawili watasimama na kuilaani nchi, kwamba mvua isinye katika siku za unabii wao. Nao wataagiza moto kutoka mbinguni, na cho chote kile. Wewe ngojea. Tuna mengi sana yaliyopo hapa, ghalani kwa ajili yetu, kujifunza. [Ndugu Branham alipiga mimbara mara tatu.]

87 Loo, Yeye ni Mungu mkuu iliyoje! Ni Baba mwenye rehema iliyoje! Enyi marafiki, hebu niseme jambo hili, kama mchungaji wenu. Hamtambui majaliwa mnayoishi chini yake. Hamtambui. Kuna watu wengi mashuhuri, kuna watakatifu wengi, kuna maelfu ya watu watakatifu waliokufa katika miaka iliyopita, watu waliojazwa Roho ambao wangependa kuiona siku hii mnayoishi. Hebu mimi na wewe tutumie siku hii vizuri.

Tuna jambo gani lingine la kutarajia? Tunaweza kufanya nini baada ya jambo hilo? Tunaelekea wapi? Ni kitu gani kitakachotukia? Hatuna budi kwenda mahali fulani. Huwezi kukaa hapa wakati wote. Unaweza kukata nyasi zako; juma lijalo zitahitaji kukatwa tena; naam, mara mbili, kabla ya wakati huo. Mnaweza kuwalea watoto wenu. Unawapa chakula chao cha mchana; wakati wa chakula cha jioni wana njaa tena. Wape chakula cha jioni; wanaona njaa tena asubuhi yake. Unawanunulia jozi ya viatu; kama wao ni kama wangu, kufikia kama miezi miwili ama mitatu utawanunulia pea nyingine. Unawanunulia nguo mwezi huu; baada ya mwezi mmoja ama miwili unawanunulia nguo mpya. Mnaona? Hakuna kitu cha kudumu. Hakuna kitu thabiti. Hakuna kitu kinachoweza kusimama.

Usitamani utajiri wa bure wa ulimwengu huu,
Hayo yanaoza upesi sana,
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Hawatapita kamwe!
Wakati unajazwa na tafsiri ya haraka,
Hakuna kitu duniani kisichotikisika kinachoweza kusimama,
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Sikilizeni!

Wakati safari yetu itakapokamilika, (Yeye atatujulisha itakapokwisha.)
Kama tumekuwa waaminifu kwa Mungu,
Nyumba yetu ni nzuri na yenye utukufu huko Utukufuni, (huo Mji uliotiwa mafuta)
Nafsi zetu zilizoshangilia zitatazama!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Usitamani utajiri wa bure wa ulimwengu huu,
Hayo yanaoza upesi sana,
Jenga tu matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Hawatapita kamwe!

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Wakati tumeinamisha vichwa vyetu. Kama hujapata kuuchukua Mkono Wake, mbona usije ufanye jambo hilo sasa.

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

88 Ewe msichana mdogo, wewe kisichana kirembo sasa. Maskini nywele zako ni nzuri, mashavu yako ni mekundu. Lakini, unajua, itakuwa ni kesho tu, hata kufikia kuchakaa. Tunajuaje ni juma lijalo tu mabuu yatakuwa yanakutafuna, ardhini, maskini mashavu hayo mazuri mekundu?

Ewe ndugu mdogo, wewe u nguvu, ni mkubwa, mwenye misuli yenye nguvu; una matumaini makubwa. Lakini baada ya kitambo kidogo, kesho tu, nywele hizo nzuri za kipilipili zitang'oka, na ulichosalia nacho itakuwa mvi. Mabega hayo makubwa, yaliyonyooka yatainama chini, na mabuu yataanza kuyala katika mikono na katika mwili. Watakuchukua, wakulaze mavumbini.

Kwa hiyo, jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Hawatapita kamwe!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia kwa Mungu …

Ninataka uinue mkono wako na kuushika mkono Wake sasa.

Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Ndipo safari hii itakapokamilika, (itakuwa, siku moja)
Kama umekuwa mwaminifu kwa Mungu,
Nyumba yako ni nzuri na yenye utukufu,
Nafsi yako iliyochangamka itaona!
Mbona usiushikilie mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

89 Nimeona vituko vingi, karibu miaka thelathini na moja nyuma ya dawati. Nimeona vituko vya kusikitisha; Nimeona mambo mazuri sana. Jambo la kuhuzunisha sana nililopata kuona maishani mwangu… Kadiri ambavyo nimewaona watoto wakifa kwa njaa mitaani; nimewaona akina mama wakiomba kipande kimoja cha mkate. Jambo la kuhuzunisha sana nililopata kuona, ni kuona mtu, mwanadamu, na ambaye angepaswa kuwa mwana wa Mungu, akifa bila kumjua Mungu.

90 Ninamkumbuka mwanamke mmoja akiwa amesimama mlangoni usiku mmoja, mlangoni mwa kanisa hili, akanichekelea. Kisha akasema, "Nisingemruhusu ng'ombe wangu awe na aina ya dini aliyonayo!" Chini ya saa moja, niliitwa hospitalini. Mwanamke mrembo, mwenye umri wa kama miaka ishirini na miwili, alikuwa akipaza sauti, "Mlete mhubiri huyo hapa!" Alikuwa Mkatoliki, kwa imani.

Nilipoenda kule, yule mwuguzi akasema, "Umeisha chelewa, Ndugu Branham. Alikufa kama dakika tano zilizopita."

Nikasema, "Naweza kumwona?"

Akasema, "Alikuita kwa sauti kuu sana, katika maneno yake ya mwisho, 'Mwiteni yule mhubiri, Ndugu Branham!"

Mumewe alikuwa pale, akilia, "Sema sala kwa ajili yake! Sema sala!"

Nikasema, "Tumeisha chelewa sasa."

Nikaondoa blanketi kidogo. Alikuwa na macho makubwa sana ya hudhurungi. Mwanamke mwenye sura nzuri; madoadoa madogo usoni kote; nywele za hudhurungi; anavutia sana. Alikuwa amepata maumivu sana hata madoadoa yalijaa uso wake kama vipele. Macho yake yalikuwa yametokeza nje moja kwa moja kutoka kwenye vitundu vyake, namna hiyo. Na, bila shaka, matumbo yake na figo vilikuwa vimepata njia, jambo ambalo katika ninii—katika ninii… Kila mtu hufanya hivyo anapokufa, mara nyingi. Naye alikuwa hapo, amelala katika hali hiyo, mdomo wazi. Na kope zake hapa, zilikuwa zimefunika nusu ya sehemu ya hudhurungi ya jicho lake. Sitasahau kamwe. Wimbo huo uliingia moyoni mwangu.

Usitamani mali ya bure ya ulimwengu huu, uzuri, fahari.

91 Nilisimama karibu na mtu papa hapa Port Fulton, aliyekuwa anakufa. Waliniita kwenda kwenye kitanda

chake. Nami niliomba pamoja naye hapa madhabahuni usiku mmoja. Akamkumbatia mwanamke. Nikasema, "Ondoa mkono wako kwa mama huyo."

Akasema, "Ninamwongoza kwa Mungu."

Nikasema, "Si ukimkumbatia." Siamini katika upuuzi kama huo. Alinikasirikia. Akatoka kwa hasira akaenda zake.

Nilimwendea, baadaye kidogo, alipokuwa anakufa. Aliniangalia usoni, akasema, "Usiniombee, Ndugu Bill. Nimepotea. Nimepotea." Kasema, "Yote niliyowahi kupata, yamekwisha."

92 Nilisimama papa hapa pembeni, mbali kidogo na hapa, siku moja, kutoka kwa mtu aliyeniita niende karibu na kitanda chake alipokuwa anakufa. Akasema, "Daima nilitaka *kadha* na *kadha*, na *kadha.*" Yeye alisema, "Lakini kamwe sikumtumikia Bwana. Mara nyingi nimejizuia kwenda madhabahuni." Akasema, "Ndugu Branham, omba ya kwamba Mungu atamjalia msichana wangu mdogo kulipia mambo ambayo nimetenda. Labda anaweza kumfanyia Bwana jambo fulani."

Nikasema, "Hilo haliwezekani, ndugu. Mambo ambayo ungalifanya yamepotea." A-ha!

93 Nilisimama karibu na mtu, nikamwona akipigana na pepo kwa saa ishirini na nne. Kasema pepo walikuwa wamesimama karibu na kitanda chake huku wamefunga minyororo shingoni mwao. Kasema, "Msiwaruhusu wanichukue!" Akilia kwa sauti kuu; wakamshikilia kitandani. Kasema, "Huyo hapo amesimama. Hummwoni? Linakuja kunichukua." Alimkatalia Mungu, kwa muda mrefu kupita kiasi. Alikuwa na maghala makubwa yaliyojaa majani ya ng'ombe, yamejaa ngano, farasi wazuri wa mashindano. Mwaka mmoja kabla ya hapo, alimtukana Mungu mbele ya uso Wake; akampiga kofi mkewe kwa ajili ya kwenda maskanini. Mnajua kilichotukia? Umeme ulipiga ghala lake, na ukaua farasi wake, ukachoma nyasi zake. Na mtu huyo akafa katika namna fulani ya kupunga pepo, akipigana na pepo wamwache.

94 Na rafiki msiri wangu (utukufu!) amesimama kule ng'ambo, alifikia mwisho wa safari yake. Nikasema, "Je! unaondoka, baba?"

Kasema, "Hili ndilo jambo lenyewe, Billy."

Nikasema, "Wasikiaje?"

Akasema, "Yote ni shwari." Kasema, "Walete watoto wangu karibu na kitanda changu." Akaweka mikono yake minyonge juu ya kila mmoja wa watoto wake akawabariki. Akawaambia wanawe wawili, kasema, "Shikilieni mikono yangu, iinueni juu, kama Yoshua na Kalebu walivyofanya." Nikashangaa alichokuwa anataka kusema. Akasema:

Siku ya furaha, siku ya furaha,
Tangu Yesu alipoziosha dhambi zangu!
Yeye alinifundisha jinsi ya kukesha na kuomba,
Na kuishi kwa furaha kila siku.

Tuna baadhi ya mambo hayo ya kufikia, marafiki! Hakuna mtu asiyetaka kula chakula kizuri, kuendesha motokaa nzuri, awe na vitu bora sana tuwezavyo kuwa navyo. Simlaumu. Hilo ni sawa. Mungu anakutaka upate hivyo.

Lakini, usitamani utajiri wa bure wa ulimwengu huu,
Hayo yanaoza upesi sana,
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Hawatapita kamwe!

Hebu na tuinue mikono yetu sasa tunapoimba.

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

95 Wakati tumesimama, hebu na tugeuke tusalimiane kwa mikono na mtu fulani sasa. Tutaendelea, na ibada, kwa muda kidogo tu. Lakini nawatakeni mgeuke tunapoimba aya nyingine ya wimbo huo.

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Fanya hivyo, baba! Fanya hivyo, baba! Kwa Mungu! Fanya hivyo, tineja! Fanya hivyo, ndugu! Fanya hivyo, ndugu!

Jenga matumaini yako katika mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

96 Hivi hamna furaha kwa ajili Yake? Sema "Amina!" [Kusanyiko linasema, "Amina!" — Mh.] Wote wampendao, waseme, "Bwana asifiwe." ["Bwana asifiwe!"] Wote wanaomini ya kwamba mnaelekea kwenye Mji huo wenye miraba minne, inua mkono wako. (Ishikilie, kwa dakika moja, pamoja na wimbo

wako.)

Ninaelekea kwenye Mji huo mzuri, (Huo unaendaje sasa?)
Bwana amewaandalia walio Wake;
Ambapo watu wote waliokombolewa wa nyakati zote
Imba utukufu kwenye Kiti Cheupe cha Enzi.
Wakati mwingine ninatamani sana Mbinguni,
Nami nitauona huo utukufu.
Itakuwa furaha ya jinsi gani,
Nitakapomwona Mwokozi wangu
Katika ule Mji mzuri wa dhahabu.

Hampendi hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Ninaelekea kwenye Mji huo mzuri,
Bwana Wangu amewaandalia walio Wake;
Ambapo watu wote waliokombolewa wa nyakati zote
Tutaimba utukufu kwenye Kiti Cheupe cha Enzi.
Loo, wakati mwingine ninatamani Mbinguni,
Na furaha nitaziona kule.
Itakuwa furaha ya jinsi gani,
Nitakapomwona Mwokozi wangu
Katika ule Mji mzuri wa dhahabu.

Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Kisha chukua Jina la Yesu,
Mwana wa huzuni na wa huzuni;
Itakupa furaha na faraja,
Chukua kila mahali uendapo.
Jina la thamani (Jina la thamani), Loo ni tamu jinsi gani! (Loo ni tamu jinsi gani!)
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani (Jina la thamani), Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Sasa, msisahau Jumapili ijayo asubuhi, saa tatu na nusu. Na ndipo tutajaribu, Bwana akipenda, kumaliza kwa wakati, kuwaombea wagonjwa, Jumapili ijayo asubuhi saa tatu na nusu.

Kwa Jina la Yesu kuinama,
Akisujudu miguuni Pake,
Mfalme wa wafalme Mbinguni tutamvika taji,
Wakati safari yetu itakapokamilika.
Jina la thamani (Jina la thamani), Loo ni tamu jinsi gani! (Loo ni tamu jinsi gani!)

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;

Jina la thamani (Jina la thamani), Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Sikilizeni tu aya hii:

Kwa Jina la Yesu kuinama,
Kama ngao toka kwa kila mtego;
Majaribu yanapokutanika,
Vuta tu Jina hilo takatifu katika maombi. (Hiyo itafanya hivyo!)
Jina la thamani (Jina la thamani), Loo ni tamu jinsi gani! (Loo ni tamu jinsi gani!)
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani (Jina la thamani), Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Sasa ninamwachia mchungaji ibada, Ndugu Neville, apate maneno yake ya kumalizia na chochote anachoweza kusema.

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7